# KANISA LA BIBLIA

Na

J. C. Choate

Kimechapishwa na

World Literature Publications
Winona / Singapore / New Delhi / Cape Town

Niim Computers & Graphics (T)
Dar es Salaam - Tanzania

Wasiliana na: Bright Mwakaboko
E-mail: mwakaboko87@gmail.com
au piga simu +255(0)758 310 304

**Wafasiri:**
Godfrey Wallace
Bright Mwakaboko

Kimetafsiriwa 2015

**HAKIUZWI**

## MWONGOZO KWA WOTE WANAO PENDA KUTUMIA KITABU HIKI KAMA MAFUNZO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA.

Tafadhali soma kifaa hiki kiukamilifu, pamoja na Biblia yako au Agano Jipya, na kisha chukua karatasi lako na ujibu maswali, somo baada ya somo. Hakikisha umeonyesha juu ya karatasi kuwa maswali yaliyojibiwa ni ya somo la kwanza, somo la pili, au somo lolote unalofanya kwa wakati huo. Kitunze kitabu chako salama, na utume majibu uliyoandika katika kila sura. Utataka kukabidhi majibu ya masomo ma nne au matano kwa wakati mmoja. Yapewe maksi na yarudishwe kwako, na kisha endelea hadi utakapo maliza kitabu. Hongera kwa kuchukua mfululizo wa masomo, na ufaidi sana kwayo.

***Mwandishi***

Copyright 1998, J.C. Choate Publications.

Mara ya kwanza kuchapishwa kwa Kiswahili, 2016.

Kimechapishwa ndani ya India, Sri Lanka, Pakistan, Indonesia, Singapore, Guatemala, Russia, Ghana, South Africa, Korea, Phillippines, U.S.A., na Tanzania.

Zaidi ya 100,000 vimeshachapishwa na kusambaa ulimwenguni kote.

Kimechapishwa katika Kiingereza, Kihindi, Kipaite, Kiurdu, Kitelugu, Kikorea, Kizulu, Kijapani, Kitamil, Kimalayalam, Kiindonesia, Kichina, Kispanish, Kirusi, Kibengali, Kifaransa, Kipunjabi, na Kiswahili.

Vimechapwa vitabu 2,000 copies, 2016.

Agiza kutoka:

J.C. Choate Publications

PO Box 72

Winona, MS 38967

Email: choate@worldevangelism.org

**Tanzania:**

Wasiliana na: Bright Mwakaboko
E-mail: mwakaboko87@gmail.com
au piga simu +255(0)758 310 304

# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| *Somo la Kwanza* - Maana ya kanisa | 1 |
| *Somo la Pili* - Kuja kwa kanisa | 9 |
| *Somo la Tatu* - Kuanzishwa kwa kanisa | 17 |
| *Somo la Nne* - Utambulisho wa kanisa | 27 |
| *Somo la Tano* - Jina la kanisa | 35 |
| *Somo la Sita* - Muundo wa kanisa | 45 |
| *Somo la Saba* - Kuingia ndani ya kanisa | 53 |
| *Somo la Nane* - Ibada ya kanisa | 61 |
| *Somo la Tisa* - Kazi ya kanisa | 69 |
| *Somo la Kumi* - Umoja wa kanisa | 79 |
| *Somo la Kumi na Moja* - Fundisho la kanisa | 87 |
| *Somo la Kumi na Mbili* - Historia ya kanisa | 95 |
| *Somo la Kumi na Tatu* - Kanisa leo | 105 |
| *Majibu* – Somo la Kwanza hadi Somo la Kumi na Tatu | 114 -139 |

# UTANGULIZI

Niliandika kifaa hiki kwanza kama masomo ya Biblia kwa njia ya Posta na kilionekana kwa majuma 13, somo moja kwa muda katika gazeti la wiki ndani ya Colombo, Sri Lanka. Tangu wakati ule mawazo yalilenga wale wote wasiolijua kanisa la Bwana, nilijitahidi kuyarahisisha masomo haya iwezekanavyo. Somo lolote linalofuata juu ya somo linaonyesha somo lililopita, na kisha maswali yalifuata kila somo, pamoja na pointi kuu zote zikiwa tayari. Baada ya kwenda New Delhi, India, tulikuwa tunakozi imekwisha kuchapwa katika mfumo wa kitabu. Ikachapishwa tena kule katika lugha nyingi na zinaendelea kutumika hadi leo hii. Baadaye, ilichapishwa ndani ya Sri Lanka, Singapore, Guatamala, huku USA, na katika nchi zingine nyingi. Kimetumika sio tu katika nchi hizi bali kimetumwa kwa watu tuliowasiliana nao na kwa Wakristo ulimwenguni.

Lengo la hiki kitabu ni kumtambulisha msomaji kanisa la Biblia. Mimi binafsi naamini kwamba kama utapitia masomo haya, pamoja na Biblia yako, utaamini kwamba Bwana ana kanisa moja tu, ambalo huvaa jina lake, na kwamba unatakiwa kuwa mshiriki wake. Lakini usichukue maneno yangu ili kuliamini. Soma na jifunze mwenyewe, binafsi, kama ndiyo kweli, kisha likubali. Kama sio kweli kataa. Hiyo ndiyo njia pekee unaweza kuwa sahihi.

Napenda kuwa hamasisha Wakristo kutumia hiki kitabu kulitambulisha kanisa la Bwana kwa marafiki zao. Kitumieni panapo bidi na naamini kitafanya mazuri.

Natazamia kuchapa vingi baadaye na naomba kwamba hiki kitabu kinaweza kutumika kuzisaidia roho nyingi kwa Kristo.

J. C. Choate

Winona, Mississippi, U.S.A.

Oktoba, 1996.

**Ukumbusho:** Shukrani kwa Makanisa ya Kristo Marekani kwa kufanya uchapishaji uwezekane.

Kitabu hiki hakijaandikwa kwa kuibadili Biblia.
Hiki kitabu ni kwa msaada wako tu.

# 1

## SOMO LA KWANZA

# MAANA YA KANISA



Hakuna mtu yeyote atayekataa kwamba Biblia inazungumza kuhusu kanisa. Lakini kanisa la nani? Kanisa lipi? Kanisa gani? Maswali haya na mengine mengi, yatajibiwa kadri tutakavyoendelea kuichunguza Biblia katika huu mfululizo wa haya masomo yetu.

Tuanze kwa kuelezea jinsi kanisa lilivyoelezewa katika Biblia, kanisa sio Katoliki, wala dini ya uyahudi. Kanisa sio dhehebu, au umoja wa madhehebu, au ulokole wa kimadhehebu. Kanisa sio taasisi ya kisiasa, kama vile taasisi zingine za kijamii, na wala sio nyumba ya kuleta malighafi. Hivyo basi kama kanisa sio mojawapo wa haya yote. Hivyo sasa kanisa ni nini?

Idadi kubwa ya watu hawaelewi maana halisi ya neno kanisa, kwa sababu hawajafanya utafiti katika Biblia. Matokeo yake, hawaelewi kusudi la kanisa, umuhimu wa kanisa, na kazi ya kanisa. Lakini kwa uwazi kabisa Biblia inatuambia au inatueleza maana halisi ya neno kanisa. Neno kanisa limetoka katika neno la kiyunani *ekklesia*, linalomaanisha "walioitwa kutoka." Hivyo kanisa ni kundi la watu walioitwa, wale ambao wameitwa kutoka katika dunia na kuingia katika ufalme wa Mwana mpendwa wa Mungu (Kolosai 1:13). Ni mwili wa kiroho wa Kristo (1 Korintho 12:27), ni jumuia ya wale wote walio mtii Kristo (Waebrania 5:8-9), na kwa hiyo wanaokolewa na yeye na kuongezwa katika kanisa lake (Marko 16:16; Matendo 2:47). Njia nyingine ya kulielezea, kanisa lina wafuasi wa Yesu.

Neno kanisa limeonekana katika Biblia katika dhana mbili. Kwanza Biblia imeizungumzia kanisa katika dhana

ya ujumla. Hili ndilo ambalo Yesu alikuwa nalo akilini aliposema, “Nami nakuambia, wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu, wala milango ya kuzimu haitalishinda” (Mathayo 16:18). Kuna mistari mingine mingi ambayo neno kanisa limetumika katika njia hiyo hiyo, kuzungumza kuhusu kanisa katika dhana ya ujumla, inamaana, mahali popote ambapo kanisa litaonekana duniani, kama ni kanisa la Biblia, ni lile kanisa ambalo Yesu alisema atalijenga. Pili, kanisa limezungumziwa katika dhana maalum. Kwa mfano, Paulo alipokuwa akiwaandikia walio mtii Kristo kule Rumi, yaani kanisa lililokuweko Rumi na kuzungumza na makusanyiko tofauti tofauti, alisema, “Makanisa yote ya Kristo yawasalimu” (Warumi 16:16). Hakuwa akizungumza kuhusu idadi ya makanisa, katika dhana ya madhehebu, lakini kiasi cha idadi ya makusanyiko husika ya kanisa la Bwana au kanisa la Kristo.

Kwa kufafanua zaidi, utagundua kwamba maandiko yanazungumza kuhusu kanisa la Korintho, kanisa la Waefeso, kanisa la Filipi, nk. (1 Korintho 1:2; Waefeso 1:1; Wafilipi 1:1). Yote haya yanawachanganya baadhi ya watu kwa sababu wamezoea kufikiri kanisa katika hali ya udhehebu tu. Lakini hautasoma kuhusu dhehebu la kwanza katika neno la Mungu. Katika hali ya kuendelea kuna idadi ya makusanyiko yaliyozungumziwa na kila kusanyiko ni Kanisa la Bwana la mahali pamoja, lakini yote kwa pamoja hujumuisha Kanisa kwa ujumla. Ni rahisi sana kuacha dhehebu na kuiendea Biblia na kuliona kanisa kama Bwana alivyolitoa.

Kwa kutusaidia zaidi kuelewa maana ya kanisa katika uhalisia wake, hebu tuangalie kwamba Biblia inaliona kanisa kama:

1. **Mwili wa Kristo.** Ni mwili wa kiroho wa Kristo, likiwa na Kristo akiwa kichwa cha kanisa (Waefeso 5:23). Hakuna zaidi ya mwili mmoja (Waefeso 4:4), na mwili mmoja ni kanisa moja (Wakolosai 1:18)
2. **Nyumba ya Mungu.** Neno nyumba katika maandiko yanamaanisha familia, ambayo inatusaidia kuelewa kuwa kanisa ni familia ya Mungu. Katika 1 Timotheo 3:15 Paulo anasema kuwa nyumba ya Mungu ni kanisa la Mungu aliye hai. Mungu ni Baba na sisi ni watoto wake (Wagalatia 3: 26,27; Waefeso 1:3).
3. **Ufalme wa Mungu.** Ufalme unamaanisha mfalme, na hivyo Kristo ndiye mfalme (Ufunuo 17:14). Lakini ili kuwe na mfalme, ufalme unatakiwa uwepo sasa, na upo (Matendo 8:12). Sisi ni raia wake, dunia ni nchi yake, na Agano Jipya ni sheria yake. Hakika, hili ndilo kanisa ambalo Bwana aliliahidi (Mathayo 16:18,19).
4. **Shamba la Bwana.** Kristo ni mzabibu na Mkristo mmoja mmoja ni tawi (Yohana 15:1-8). Wazo hapa ni kufanya kazi katika shamba la mzabibu na kuzaa matunda kwa ajili ya Bwana.

Kanisa ndivyo lilivyofafanuliwa katika maandiko. Tafadhali jifunze kuhusu maada hizi katika mwanga wa maandiko na ujionee mwenyewe. Kama utaliona kanisa kama Mungu alivyotarajia wewe ulione, basi fikra zako zote zitabadilika, na labda hata maisha yako.

# MASWALI YA KUJIFUNZA

## Somo la Kwanza

***Tafadhali chora duara kwenye jibu sahihi:***

| | | |
|---|---|---|
| NDIYO | HAPANA | 1. Biblia inazungumzia kuhusu kanisa. |
| NDIYO | HAPANA | 2. Kanisa ni Katholiki. |
| NDIYO | HAPANA | 3. Watu wengi wanalielewa kanisa. |
| NDIYO | HAPANA | 4. Neno kanisa limetumika katika Biblia katika dhana moja tu. |
| NDIYO | HAPANA | 5. Kristo alisema atajenga makanisa yake. |
| NDIYO | HAPANA | 6. Makanisa saba ya Asia ni madhehebu saba tofauti (Ufunuo 2,3). |
| NDIYO | HAPANA | 7. Kanisa ni mwili wa Kristo. |
| NDIYO | HAPANA | 8. Kuna mwili mmoja. |
| NDIYO | HAPANA | 9. Kristo ndiye kichwa cha kanisa. |
| NDIYO | HAPANA | 10.Ufalme bado haujaja. |

***Tafadhali toa jibu lililo sahihi:***

1. Orodhesha vitu ambavyo kanisa sio.

2. Kanisa limetoka katika neno gani la Kiyunani?

3. Kanisa lina vitu gani?

4. Ni dhana zipi mbili ambazo kanisa limetumia?

5. Ni nani alisema atalijenga kanisa lake?

6. Alijenga makanisa mangapi?

7. Makanisa saba yaliyoko Asia ni makanisa yapi?

8. Kuna miili mingapi?

9. Mfalme wa Wafalme ni nani?

10. Tunapaswa kufanya nini katika shamba la Bwana la mizabibu?

***Tafadhali toa maelezo mafupi:***

1. Ekklesia

2. Mwili wa Kristo

3. Nyumba ya Mungu

4. Ufalme wa Mungu

5. Shamba la mizabibu la Bwana

## *SEHEMU YA KUANDIKIA VITINI*

# 2

## SOMO LA PILI

# KUJA KWA KANISA



Kanisa halikuja kwa usiku mmoja. Kanisa lilipangwa, lilitabiriwa, liliahidiwa, na baadae likaanzishwa.

Kwanza, kanisa lilikuwa katika akili ya Mungu. Paulo analieleza hili kwa watakatifu walioko Waefeso. Anasema, "*Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo; kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika pendo. Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi yake. Na usifiwe utukufu wa neema yake, ambayo ametuneemesha katika huyo mpendwa*" (Waefeso 1:3-6). Tafadhali zingatia kwamba anazungumza na kanisa lililoko Waefeso na anasema Mungu amewachagua wao kabla ya misingi ya ulimwengu. Hii inamaana kwamba Mungu alifikiri kuhusu kanisa hata kabla ya kuumbwa kwa ulimwengu. Ina maana kwamba alipanga wakati huo, na hivyo lilianzia katika mawazo ya Mungu. Ni jambo la kipuuzi kiasi gani, tena kudhalilisha na kutoa thamani kile ambacho Mungu amepanga tangu mwanzo.

Pili, kanisa lilizungumziwa katika unabii katika matukio tofauti tofauti. Isaya alisema, "*Na itakuwa katika siku za mwisho, mlima wa nyumba ya Bwana utawekwa imara juu ya milima, nao utainuliwa juu ya vilima; na mataifa yoye yatauendea makundi makundi. Na mataifa mengi watakwenda na kusema,njooni, twende juu mlimani kwa Bwana, nyumbani kwa Mungu wa Yakobo, naye atatufundisha njia zake, nasi tutakwenda katika mapito yake maana katika Sayuni itatoka sheria na neno la*

*Bwana katika Yerusalemu*" (Isaya 2:2-3). Yoeli alisema, "*Hata itakuwa, baada ya hayo, ya kwamba nitamimina Roho yangu juu ya wote wenye mwili; na wana wenu waume kwa wake, watatabiri,wazee wenu wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono; tena juu ya watumishi wenu, wanaume kwa wanawake katika siku zile, nitamimina Roho yangu*" (Yoeli 2:28-29). Halafu Danieli akaonesha, "*Na katika siku za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele, wala wengine hawataachiwa enzi yake; bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele*" (Danieli 2:44).

Sasa tuangalie baadhi ya hitimisho:

1. Ufalme utaanzishwa katika siku za mwisho.
2. Ufalme utaanzishwa katika milima.
3. Mataifa yote watauendea.
4. Bwana atamwaga Roho yake katika miili yote.
5. Litaanzishwa katika siku za ufalme wa nne wa dunia.
6. Utameza falme nyingine zote na kusimama milele.

Sasa, haya yote yalitimizwa wapi? Soma kitabu cha Matendo sura ya 2.

Tatu, kanisa liliahidiwa. Yohana alisema unakaribia (Mathayo 3:2). Ina maana kwamba ulikuwa karibu au utaanzishwa karibuni. Kristo aliahidi, "*Nami nakuambia, wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda*" (Mathayo 16:18). "*Akawaambia, amin, nawaambia, pana*

*watu katika hawa wasimamao hapa, ambao hawataonja mauti kabisa, hata watakapouona ufalme wa Mungu umekuja kwa nguvu*" (Marko 9:1). "*Akawaambia, ndivyo ilivyoandikwa kwamba, Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu; na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanzia tangu Yerusalemu. Nanyi ndinyi mashahidi wa mambo haya. Na tazama nawaletea juu yenu ahadi ya baba yangu; lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu*" (Luka 24:46-49).

Hebu chunguza ukweli huu:

1. Ufalme ulikuwa karibu.
2. Kristo aliahidi kulijenga bila kujali kifo.
3. Baadhi ya wale waliokuwa na Kristo watakuwa bado hai wakati wa kulianzisha.
4. Utakuja kwa nguvu.
5. Toba na msamaha wa dhambi utahubiriwa kwa jina lake kati ya mataifa yote.
6. Utaanzia Yerusalemu.
7. Mitume watapokea nguvu toka juu katika mji wa Yerusalemu.

Tafadhali zingatia mambo haya akilini tunapofika katika kuanzishwa kwa kanisa na utaona yote haya yametimia.

Rudi sasa katika Matendo 2. Kwa kufanya hivyo, soma kwa uangalifu mara kadhaa. Mwanafunzi yeyote wa Biblia anakubali kuwa kanisa lilianza kipindi hiki. Zaidi ya yote, mahali palikuwa ni Yerusalemu kipindi kilikuwa siku za mwisho, siku za wafalme wa utawala wa Rumi,

nguvu zilikuja, toba na msamaha wa dhambi ulihubiriwa kwa mataifa yote, na kanisa likawepo tangu kipindi hicho. Hivyo, kanisa lile ambalo Mungu alikuwa nalo akilini lilianzishwa, unabii kuhusu kanisa ulitimilizwa, na ahadi kuhusu kanisa zilitimizwa.

### *SEHEMU YA KUANDIKIA VITINI*

# MASWALI YA KUJIFUNZA

## Somo la Pili

***Tafadhali toa jibu lililo sahihi:***

1. Ni wapi ambapo kanisa lilikuwepo kwa mara ya kwanza?

2. Ni lini Mungu alilichagua kanisa?

3. Taja manabii watatu ambao walizungumza kuhusu kuja kwa ufalme.

4. Ufalme utasimama kwa muda gani?

5. Ni nani aliahidi kulijenga kanisa?

6. Aliahidi kulijenga kanisa la nani?

7. Alisema atajenga makanisa mangapi?

8. Ufalme utakuja na nini?

9. Ni kitu gani kitahubiriwa Yerusalemu?

10. Ni wapi unaweza kusoma kuhusu kuanzishwa kwa kanisa?

***Tafadhali chora duara kwenye kweli au si kweli:***

KWELI SI KWELI 1. Kanisa lilipangwa, lilitabiriwa, liliahidiwa, halafu ndiyo likaanzishwa.

KWELI SI KWELI 2. Kanisa asili yake ni katika mawazo ya Mungu.

KWELI SI KWELI 3. Yohana alisema ufalme umekaribia.

KWELI SI KWELI 4. Ufalme utakuja kwa nguvu.

KWELI SI KWELI 5. Toba na ondoleo la dhambi litahubiriwa kwa jina lake katikati ya mataifa.

KWELI SI KWELI 6. Kanisa litaanzia Yerusalemu.

KWELI SI KWELI 7. Matendo 2 inatueleza kuhusu kuanza kwa kanisa.

KWELI SI KWELI 8. Hii ilikuwa ni siku za ufalme wa utawala wa Rumi.

KWELI SI KWELI 9. Siku za mwisho tayari zimeshaanza.

KWELI SI KWELI 10. Unabii na ahadi zilitimizwa na kutunzwa.

***Malizia tafadhali:***

1. "Kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla .............

   ..........................................................................................

2. "Hata itakuwa katika ..................................................

   ..........................................................................................

3. "Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao

   ..........................................................................................

   ..........................................................................................

4. "Nitalijenga ............................................................

   ..........................................................................................


5. "Toba na ondoleo la dhambi litahubiriwa, kuanza tangu.....................................................................

   ..........................................................................................

# 3

## SOMO LA TATU

# KUANZA KWA KANISA



Katika somo letu lililopita tumegundua kuwa katika kitabu cha Isaya 2:2-3; Yoeli 2:28-29; na Danieli 2:44 ufalme wa Bwana (au kanisa) utaanzishwa katika siku za mwisho, huko Yerusalemu, katika kuja kwa roho, na kila taifa litaufuata, na kwamba utasimama milele. Tena Yesu akaahidi katika Mathayo 16:18; Marko 9:1; na Luka 24:46-49 kwamba atalijenga kanisa lake, na kwamba litakuja kwa nguvu, na toba na ondoleo la dhambi litahubiriwa kwa jina lake katika mataifa yote. Sasa kwa kufungua kitabu cha Matendo 2 tutagundua kwamba ni katika sura hii tu utabiri wote umetimizwa na ahadi zote hizi zimetimilizwa.

Tunaposoma kitabu cha Matendo 2 tunaona kuwa mitume walikuwa katika mji wa Yerusalemu kipindi hicho: "*Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja. Kukaja ghafula toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Kukawatokea ndimi zilizogawanyika, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa roho mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka. Na walikuwako Yerusalemu Wayahudi wakikaa, watu watauwa, watu wa kila taifa chini ya mbingu. Basi sauti hii iliposikiwa makutano walikutanika, wakashikwa na fadhaa, kwa kuwa kila mmoja aliwasikia wakisema kwa lugha yake mwenyewe"* (Matendo 2:1-6).

Ushahidi unaendelea kutueleza kuhusu mataifa mengi ambayo yalikuwepo, "*Wakashangaa wote wakaingiwa na shaka, wakaambiana, maana yake nini mambo haya? Wengine walidhihaki, wakisema wamelewa kwa mvinyo mpya. Lakini Petro alisimama pamoja na wale kumi na*

*mmoja, akaanza kupaza sauti yake, akawaambia, enyi watu wa Uyahudi, na ninyi nyote mkaao Yerusalemu, lijueni jambo hili, mkasikilize maneno yangu. Sivyo mnavyodhani; hawa watu hawakulewa, kwa maana ni saa tatu ya mchana. Lakini jambo hili ni lile lililonenwa na nabii Yoeli: Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho yangu, na wana wenu na binti zenu watatabiri; na vijana wenu wataona maono; na wazee wenu wataota ndoto. Na itakuwa kila atakayeliitia jina la Bwana ataokolewa*" (Matendo 2:12-17,21).

Baada ya kuonesha yale yote yaliyotokea yalikuwa katika utimilifu wa unabii wa zamani, Petro alieleza katika hotuba yake. Anaonesha jinsi Yesu alivyokuwa mwanadamu amehakikishwa na Mungu katikati yao kwa miujiza na maajabu na ishara ambazo Mungu alizifanya katikati yao. Tena anatueleza jinsi gani Yesu alivyochukuliwa na kupelekwa katika baraza kwa mikono miovu alisulubiwa na kuuawa. Pia anaonesha kuwa Mungu alimfufua, akilegeza maumivu ya kifo. Ili kushawishi hadhira yake anamnukuu Daudi ili kuonesha kuwa Kristo aliishi, alikufa, alizikwa na kufufuka, tena akapaa mbinguni kukaa katika kiti cha enzi katika mkono wa kuume wa Mungu.

Kwa kuendelea, alisema, "*Yesu huyo Mungu alimfufua, na sisi sote tu mashahidi wake. Basi yeye, akiisha kupandishwa hata mkono wa kuume wa Mungu, na kupokea kwa Baba ile ahadi ya Roho Mtakatifu, amekimwaga kitu hiki mnachokiona sasa na kukisikia. Maana Daudi hakupanda mbinguni; bali yeye mwenyewe anasema, Bwana alimwambia Bwana wangu, keti upande wangu wa mkono wa kuume. Hata nitakapowaweka adui*

*zako chini ya miguu yako. Basi nyumba yote ya Israeli na wajue yakini ya kwamba Mungu amemfanya Yesu huyo mliyemsulubisha kuwa Bwana na Kristo. Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, Tutendeje ndugu zetu? Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha roho mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie. Akawashuhudia kwa maneno mengine mengi sana na kuwaonya, akisema, jiokoeni na kizazi hiki chenye ukaidi. Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu. Wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote, Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa*" (Matendo 2:32-41,47).

Katika vifungu vya maandiko vinavyoeleza kuanza kwa kanisa la Bwana Utagundua kwamba mambo yote yalitokea Yerusalemu. Mitume walimwagiwa nguvu ya Roho Mtakatifu. Kilichotokea kilikuwa ni utimilifu wa unabii wa zamani. Petro kwa udhahiri alisema, "*Lakini jambo hili ni lile lililonenwa na nabii Yoeli*" (Matendo 2:16), kwa hiyo hakuna shaka kuhusu hilo. Zaidi ya yote, tangu manabii waliposema haya yote yatatokea katika siku ya mwisho, na tangu Petro aseme yameshatokea kama nabii alivyosema kuwa yatatokea, hivyo kanisa limeshaanzishwa katika siku za mwisho. Mataifa yote yalikuwepo katika siku hiyo kama toba na ondoleo la dhambi ilihubiriwa, na watu 3000 walitii, waliokolewa, na waliongezwa katika kanisa. Kwa hiyo Kristo alianzisha

kanisa katika mji wa Yerusalemu mwaka 33 baada ya Kristo, na kanisa limekuwepo tangu siku hiyo hadi sasa.

***SEHEMU YA KUANDIKIA VITINI***

## MASWALI YA KUJIFUNZA

### Somo la Tatu

***Tafadhali toa jibu lililo sahihi:***

1. Ni nani alisema atalijenga kanisa?

2. Ni nani alisema, “Itakuwa siku za mwisho asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho yangu?”

3. Ni nani alisema, “Na Bwana akamwambia Bwana wangu, keti katika mkono wangu wa kuume?”

4. Ni nani alisema, “Tubuni, mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi?”

5. Ni nani alisema, “Jiokoeni na kizazi hiki chenye ukaidi?”

***Taja unabii tafadhali:***

1. Ni lini ufalme wa Bwana ulianzishwa?

2. Ulianzishwa katika mji gani?

3. Ni watu wangapi wataufuata?

4. Utakuja na nini?

5. Utasimama muda gani?

***Taja ahadi tafadhali:***

1. Ni nani atalijenga kanisa?

2. Litakuja na nini?

3. Ni nini kitahubiriwa?

4. Litahubiriwa katikati ya mataifa mangapi?

5. Mambo haya yatahubiriwa katika jina la nani?

***Tafadhali jibu maswali haya kutoka katika kitabu cha Matendo 2:***

1. Ni nani walipokea Roho?

2. Ni nini dalili za kuja kwake?

3. Ni namna gani Petro aliwashawishi watu kuwa Kristo alikuwa Mwana wa Mungu?

4. A. Watu waliuliza swali gani?

   B. Na jibu gani lilitolewa?

5. Ni nani aliyewazidisha waliookolewa katika kanisa?

***Tafadhali toa maana:***

1. Kanisa

2. Unabii

3. Pentekoste

4. Toba

5. Ubatizo

# 4

## <u>SOMO LA NNE</u>

# KITAMBULISHO CHA KANISA



Utawezaje kumwelekeza rafiki yako aliyepotea kwa muda mrefu? Kiuhalisia, utakusanya alama zote za utambulisho na kuanza kutafuta. Baada tu ya kupata mtu ambaye anaendana na kitambulisho, unaweza kumkubali yeye kama ndiye ambaye ulikuwa ukimtafuta. Hata hivyo kuna makanisa mengi ulimwenguni. Mtu anawezaje kutambua kanisa la kweli kanisa halisi? Mtu anawezaje kujua kuwa ni kanisa la Kristo? Ni lazima uchukue alama zote za utambulisho na ufananishe na makanisa mengine. Pale utakapopata lile ambalo linafanana na alama za utambulisho tu utakuwa na uhakika kuwa umelipata kanisa sahihi. Lakini alama za utambulisho ni zipi? Zinapatikana wapi? Biblia ndiyo jibu.

1. **Kristo alilianzisha kanisa**. "*Nami nakuambia wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu, wala milango ya kuzimu haitalishinda*" (Mathayo 16:18).
2. **Lilianzia Yerusalemu**. Hili linaonekana katika kitabu cha Luka 24:45-49 na Matendo 2:5.
3. **Tarehe ya kuanzishwa ilikuwa mwaka 33 baada ya Kristo**. Hili pia limehusika katika Matendo 2, pamoja na kanisa kuanzishwa siku ya Pentekoste.
4. **Kanisa lilivaa jina la Yesu**. Akizungumzia kuhusu makusanyiko tofauti tofauti, Paulo aliandika, "*Makanisa ya Kristo yawasalimu*" (Warumi 16:16). Aliendelea kusema, akizungumza na kanisa lililoko Korintho, "*Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila mmoja peke yake*" (1 Korintho 12:27). Lakini mwili ni nini? Ni kanisa (Waefeso 1:22-23).

5. **Washiriki wake waliitwa Wakristo**. "*Na wanafunzi waliitwa Wakristo kwanza hapo Antiokia*" (Matendo 11:26). "*Agripa akamwambia Paulo, Kwa maneno machache wadhani kunifanya mimi kuwa Mkristo*" (Matendo 26:28). "*Lakini ikiwa kwa sababu ni Mkristo asione haya, bali amtukuze Mungu katika jina hilo*" (1 Petro 4:16). Mwisho, kumbuka, "*Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo*" (Matendo 4:12).
6. **Kristo ndiye kichwa pekee**. "*Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote*" (Wakolosai 1:18).
7. **Hakuna zaidi ya moja**. "*Mwili mmoja, na Roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu*" (Waefeso 4:4). Lakini mwili ni nini? Ni kanisa (Wakolosai 1:18). Kwa hiyo kama kuna mwili mmoja na ni kanisa, hakuna zaidi ya kanisa moja.
8. **Kuna vigezo kwa ajili ya kuingia katika kanisa**. Hii ni pamoja na imani (Waebrania 11:6), toba (Matendo 17:30), ukiri wa imani (Warumi 10:9,10) na ubatizo (Marko 16:16). Mara tu mtu anapookolewa anaongezwa katika kanisa (Matendo 2:47). Pia Warumi 6:3-4; Wagalatia 3:26-27; na 1 Korintho 12:13 zinafundisha kuwa mtu anabatizwa katika Kristo na kanisa lake. Kwa kuzitii amri hizi mtu atasema amezaliwa katika kanisa au ufalme (Yohana 3:3-5).

9. **Ibada ya kanisa ni yakipekee.** Wakristo wanatakiwa kukusanyika katika siku ya kwanza ya juma (Matendo 20:7), kuimba (Waefeso 5:19), kusali (Matendo 2:42), kujifunza (2 Timotheo 2:15), kushiriki meza ya Bwana (Matendo 20:7), na kutoa (1 Korintho 16:2).

10. **Fundisho la kanisa linatoka kwenye Biblia tu**. Linakubalika bila kuongeza, kupunguza, au kuweka kitu mbadala (Ufunuo 22:18-19). Biblia ndilo fundisho la pekee la kanisa. Vitabu vya ziada au mafundisho mengine yamekataliwa (Mithali 30:5-6).

11. **Uongozi wa kanisa lazima uwe kulingana na mpango wa Mungu.** Kristo ni kichwa (Waefeso 5:23), na kila kusanyiko lina wazee wake na mashemasi wake lenyewe (1 Timotheo 3; Tito 1). Kanisa la Bwana halina kiongozi mkuu duniani wala makao makuu na wala halina uongozi wa kibinadamu wa kitaifa au kimataifa.

12. **Kazi za kanisa ziko katika nyanja tatu zilizoshikamana**. Kanisa linafanya kazi ya kuhubiri injili (Marko 16:15-16), kuwasaidia wahitaji (Wagalatia 6; Yakobo 2), na kuwaelimisha washiriki wake (Waebrania 3:12-14).

13. **Kila Mkristo lazima aishi maisha matakatifu ya Ukristo**. Hatuwezi kuupenda ulimwengu (1 Yohana 2:15; Yakobo 4:4), lakini lazima uzae matunda ya Roho (Wagalatia 5:22-23). Ni waaminifu tu watakaopokea taji ya uzima.

Hizi ni baadhi ya alama za kanisa. Hizi zimetolewa katika kielelezo, ambacho ni Biblia. Linganisha kanisa

unalosali na kanisa hili. Kwa mfano, linganisha kuanzia namba moja hadi namba nne. Jiulize mwenyewe, “Ni nani alilianzisha kanisa ninalosali?” “Je, lilianzishwa na Kristo au mtu mwingine?” Jiulize tena, “kanisa ninalosali lilianzia wapi?” “Je, lilianzia Yerusalemu au sehemu nyingine?” Endelea kujiuliza, “Je, kanisa ninalosali lilianza lini?” Kama lilianza baada ya mwaka 33 Baada ya Kristo litakuwa si kanisa la Bwana. Mwisho, jiulize mwenyewe, “kanisa ninalosali limevaa jina la nani?” Kama si jina la Kristo, mimi nitakuwaje wa Kristo? Unaweza kuendelea, lakini haya yanatosha kukusaidia kuona kuwa kanisa unalosali ni la Bwana au la mwanadamu. Unaweza kulinganisha makanisa mengine na alama hizi za utambulisho ili uyajue kama ni ya Mungu au la. Ninaamini utaweza kuona tofauti ikiwa utajiamini mwenyewe.

Ikiwa utagundua kuwa kanisa ambalo unashiriki si kanisa la kweli la Biblia, nikusihi uliache hilo kanisa, jifunze ukweli, utii ukweli, na uzidishwe katika kanisa ambalo unaweza kulisoma katika maandiko ya Mungu. Baada ya hapo utakuwa katika kanisa ambalo wokovu unapatikana ndani yake.

# MASWALI YA KUJIFUNZA

## Somo la Tano

***Tafadhali toa majibu sahihi:***

1. Unawezaje kumwelekeza rafiki yako aliyepotea kwa muda mrefu?

2. Je, kuna makanisa ya kimadhehebu katika ulimwengu wa leo?

3. Mtu anawezaje kujua kanisa sahihi?

4. Alama za utambulisho zinapatikana wapi?

5. Ni nani alilianzisha kanisa?

6. Kanisa hilo lilianzia wapi?

7. Kanisa hilo lilianza lini?

8. Taja jina moja linalopatikana katika Biblia kuhusu kanisa hilo.

9. Mwili ni nini?

10. Washiriki wa kanisa hilo waliitwaje?

11. Kichwa cha kanisa hilo ni nani?

12. Je, kuna makanisa mangapi?

13. Taja vigezo vya kuzidishwa katika kanisa la Kristo.

14. Ni jinsi gani mtu anaweza kuingia kwa Kristo na katika kanisa?

15. Orodhesha matendo ya ibada.

16. Fundisho la kanisa ni lipi?

17. Elezea ni vitu gani ambavyo kila kusanyiko linapaswa kuwa navyo.

18. Taja kazi tatu zilizofungamana za kanisa.

19. Mkristo anapaswa kuwa na maisha ya aina gani?

20. Ni nani atakayepokea taji ya uzima?

21. Je, kanisa linaweza kuwa la Bwana ikiwa mwanadamu alilianzisha?

22. Je, kanisa linaweza kuwa la Bwana kama mwanzo wake haukuwa ni Yerusalemu?

23. Je, kanisa linaweza kuwa la Bwana kama litakuwa limeanza baada ya mwaka 33 baada ya Kristo?

24. Je, kanisa linaweza kuwa la Bwana kama washiriki wake hawatavaa jina la Kristo?

25. Ikiwa umeokoka, Kristo atakuzidisha katika kanisa gani?

# 5

## SOMO LA TANO

# JINA LA KANISA



Kama kanisa linapaswa kuwa la kimaandiko, basi ni lazima kuwa na jina la kimaandiko. Hata hivyo, kuna makanisa mengi yaliyoundwa na wanadamu, yenye majina na vyeo vya wanadamu. Hayo yote yamekujaje? Baadhi ya majina hayo yalitolewa ili kuwaenzi waanzilishi wake: kama vile "Lutheran". Baadhi huwakilishwa na mafundisho ya kiimani kama vile: ubatizo au njia ya kufanya kazi ya Bwana. Baadhi yao hutukuza siku, kama vile siku ya Pentekoste au siku ya sabato.

Bado wengine wanaweka msisitizo juu ya aina za serikali kwa kuainisha kazi za wazee wa kanisa. Lakini yote haya, na mengine yoyote ambayo yanaweza kutajwa, huchukua utukufu wote, sifa na heshima impasayo Kristo. Majina, vyeo na maelezo ambayo hutokana na wanadamu.

Vyeo na majina yatokanayo na wanadamu yanamakosa kwa sababu kadhaa; kwanza, husababisha mgawanyiko. Hufanya tofauti ambapo Mungu hakukusudia kuwa tofauti. Yanawagawa watu. Yanapinga sala ya Kristo kama inavyonakiliwa katika Yohana 17 wakati alipoomba kwamba wote na tuwe na umoja. Pili, yanakatazwa katika maandiko. Katika Wakorintho wa kwanza 1:10-17, Mtume Paulo alionyesha ndugu zake makosa ya kuvaa majina yatokanayo na watu, hivyo kugawa vyama na madhehebu. Tatu, majina yatokanayo nawanadamu huwa mbadala wa jina la Bwana. Hata hivyo, sisi tunasoma kuhusu jina la Kristo;*"Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo"* (Matendo 4:12). Nne, vyeo na majina ya kibinadamu hupotosha, huleta utata, na huunda

hisia mbaya miongoni mwa wasioamini. Husababisha kutoamini. Tano, husababisha wote ambao huyavaa kupotea. Kwa sababu hizo, ni makosa na ni dhambi. Na kwa kanisa, Kristo aliahidi kulijenga (Mathayo 16:18), na imesemwa kwamba yeye alilinunua kwa damu yake mwenyewe (Matendo 20:28), na kwamba alikuwa Mkombozi wake (Waefeso 5:23), na kichwa chake (Wakolosai 1:18). Hivyo ni kawaida tu kuvaa jina lake kwa heshima yake kama mwanzilishi wake, mjenzi wake, Mkombozi, na kichwa chake. Hivyo Paulo alipoliandikia kanisa huko Rumi, na kutuma pamoja salamu katika makusanyiko ya eneo hilo, alisema, "*Salimianeni kwa busu takatifu. Makanisa yote ya Kristo yawasalimu"* (Warumi 16:16). Tena akizungumza na kanisa la Korintho, alisema; "*Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila kimoja peke yake"* (1 Wakorintho 12:27). Lakini kwa vile kanisa ni mwili wa Kristo (Waefeso 1:22-23), alikuwa akizungumzia kanisa la Kristo. Pia liliitwa kanisa la Mungu (1 Wakorintho 1:2; Matendo 20:28), ufalme wa Mungu (1 Wakorintho 6:9), ufalme wa Kristo (Waefeso 5:5), ufalme wa Mwana wa pendo lake (Wakolosai 1:13), ufalme wa Bwana wetu (2 Petro 1:11), kanisa (Matendo 13:1), kanisa la Mungu aliye hai (1 Timotheo 3:15), kanisa la mzaliwa wa kwanza (Waebrania 12:23), nk.

Hivyo kanisa halikuitwa kwa majina ya kipekee au mafungu ya maelezo. Wakati huo huo, na ikumbukwe kwamba kile ambacho ni mali ya Mungu ni mali ya Kristo na vivyo hivyo kinyume chake. Pia hayo majina yote yanawakilisha kanisa ambalo Kristo alijenga. Kama siyo kanisa la Kristo, basi laweza kuwa kanisa la nani? Zaidi

sana, pamoja na majina yote hayo na maelezo yake ya maneno, inaweza kuonekana kuwa mtu aweza kutamani kuacha mbali maandiko na kuchagua jina jingine kwa ajili ya kanisa la Bwana. Lakini hebu na tukae pamoja na Biblia nakuita kanisa vile Biblia inavyoliita. Nasi tutakuwa katika haki.

Kuhusu majina ya washiriki wa kanisa, pia maandiko yameweka wazi. Kwa kuanzia, nabii Isaya alisema kwamba Mungu angewapa watu wake jina jipya (Isaya 62:2). Jina lilizaliwa na Paulo miaka mingi baadaye (Matendo 9:15), lakini haikupaswa kutolewa mpaka watu wa mataifa wapate nafasi ya kumtii Mungu. Yote hayo yalitimilika katika Antiokia ya siria ambako mitume waliitwa Wakristo kwa mara ya kwanza huko (Matendo 11:26). Baadaye, tunasoma ambapo Paulo alikuwa akimhubiria Mfalme Agripa, naye alijibu kwa kusema, "*Agripa akamwambia Paulo, Kwa maneno machache wadhani kunifanya mimi kuwa Mkristo* (Matendo 26:28). Mwisho, tunasoma mahali ambapo Petro alisema " *Lakini ikiwa kwa sababu ni Mkristo asione haya, bali amtukuze Mungu katika jina hilo"* (1 Petro 4:16) .

Kwa hiyo ni wazi kwamba wafuasi wa Kristo katika nyakati za Agano Jipya walikuwa ni Wakristo na Wakristo tu. Bwana angependa na tuwe hivyo leo. Kama sisi tutavaa majina na vyeo juu ya jina la Wakristo basi hiyo inamaana sisi si Wakristo wa kweli. Jina Mkristo humtofautisha mtu toka watu wa mataifa ya dunia na ni hilo tu Bwana analihitaji .

Katika yote, jina la kanisa na waumini wake, jina la Kristo lapaswa kutukuzwa. Kwa nini? Kwa sababu ni jina la

familia (Waefeso 3:14-15), jina lipitalo kila jina (Wafilipi 2:9-11), jina ambalo wokovu hupatikana kwalo (Matendo 4:12). Kwa hiyo inatupasa kuamini katika jina la Kristo (1 Yohana 5:13), kukiri kwa jina hilo (2 Timotheo 2:19), kutubu na kubatizwa kwalo (Matendo 2:38), kukutana kwa ajili ya ibada kwa jina hilo (Mathayo 19:20), fanya yote katika jina lake (Wakolosai 3:17), ili tupate uzima wa milele kwa jina lake (Yohana 20:30-31).

Tukiwa na mawazo hayo katika akili zetu, hakika hakuna mtu anaweza kusema kwamba hakuna kitu katika jina hilo. Ni hakika hakuna wokovu katika majina na vyeo vya kibinadamu, bali wale wayavaao watapotea kwa sababu yake. Kwa mana nyingine, kuna wokovu katika jina la Kristo tu.

## MASWALI YA KUJIFUNZA

### Somo la Tano

***Tafadhali kamilisha sentensi hizi:***

1. “Kanisa lazima kuwa na ____________________ la kimaandiko.

2. “Majina na vyeo vya kuwekwa na binadamu ni __________________________________na ni ______ ______________________________________________.

3. “Maombi ya _____________________” yalihimiza ______________________________________________.

4. “Sasa ninyi ni ________________________________ ______________________________________________.

5. “Mungu angewapa watu wake __________________ ______________________________________________.

*Tafadhali zungushia mduara jibu sahihi:*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | NDIYO | HAPANA | 1. | Lazima kanisa kuwa na jina la kimaandiko ili kuwa la kimaandiko? |
| 2. | NDIYO | HAPANA | 2. | Vyeo na Majina ya kibinadamu ni makosa? |
| 3. | NDIYO | HAPANA | 3. | Je, Wokovu ni katika jina la Kristo? |
| 4. | NDIYO | HAPANA | 4. | Je, Bwana angependa sote tuwe na jina moja leo? |
| 5. | NDIYO | HAPANA | 5. | Je, mtu aweza kumtukuza Bwana bila kuvaa jina lake? |

***Tafadhali toa majibu sahihi:***

1. Ni kwa namna gani baadhi ya majina ya kibinadamu yakitokea?

2. Orodhesha sababu kwa nini majina ya kibinadamu ni makosa.

3. Kristo aliombea nini?

4. Eleza Pauo alivyofanya nini alipogundua ndugu zake walikuwa wanagawanyika katika makundi.

5. Je, kwa nini kanisa linapaswa kuvaa jina la Kristo?

6. Nukuu Warumi 16:16.

7. Mwili wa Kristo ni nini katika 1 Wakorintho 12:27?

8. Toa baadhi ya majina mengine ya kanisa.

9. Kama kanisa halikuwa kanisa la Kristo, basi lilikuwa kanisa la nani?

10. Washiriki wa kanisa waliitwa nani?

11. Orodhesha maandiko matatu yanayo ongelea jina Mkristo.

12. Bwana angependa leo wote tuweje?

13. Inawezekana kuwa aina fulani ya Mkristo?

14. Kwa nini tulitukuze jina la Kristo?

15. Je, twapaswa kufanya nini katika jina la Kristo?

*SEHEMU YA KUANDIKIA VITINI*

6

## SOMO LA SITA

# MUUNDO WA KANISA



Kristo alianzisha kanisa (Mathayo 16:18). Kanisa lililoundwa na watu walioitwa, toka ulimwengumi mwote (Wakolosai 1:13-14). Linajumuisha waliookolewa (Matendo 2:47). Hivyo ni mwili wake wa kiroho (Wakolosai 1:18), na kuna kanisa moja tu (Waefeso 4:4).

Wakati kanisa lina asili ya ujumla, huundwa na mamia na maelfu ya makusanyiko binafsi, na kila kusanyiko limeundwa na washiriki wengi binafsi. Hii inamaana kwamba serikali ni ya kanisa la mahali pamoja na si ya kitaifa au kimataifa. Kwa maneno mengine, kanisa la Bwana halina kichwa duniani au makao makuu ya hapa duniani.

Maandiko hufundisha kwamba Kristo ni kichwa cha kanisa. Hebu tuchunguze mistari inayofuata; "*akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote*" (Waefeso 1:22-23). "*Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha Kanisa; naye ni Mwokozi wa mwili*" (Waefeso 5:23). "*Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote*" (Wakolosai 1:18). Sasa mistari hii hufundisha nini? Kama ilivyokwisha elezwa, kwamba Kristo ni kichwa cha mwili, ambao ni kanisa. Je kuna vichwa vingapi katika mwili mmoja? Hakika ni kimoja tu, nacho ni Kristo, na kwamba hakuna mwenye kushirikiana naye katika nafasi hiyo.

Pamoja na kuwa kanisa linafanywa na makusanyiko mengi, na kwa kuwa Kristo ndiye kichwa cha kanisa, hivyo hiyo inamaana yeye ni kichwa cha kila kusanyiko au kanisa la mahali pamoja, hata hivyo kwa kuwa yeye ni kichwa cha kila mshiriki wa kanisa. Kwa kuzingatia hili, Paulo alisema, "*Lakini nataka mjue ya kuwa kichwa cha kila mwanamume ni Kristo, na kichwa cha mwanamke ni mwanamume, na kichwa cha Kristo ni Mungu"* (1 Wakorintho 11:3).

Tena, kila kusanyiko la mahali pamoja litakuwa na muundo wake wa uongozi. Pamoja na Kristo kuwa kichwa, watakuwepo miongoni mwa washiriki waliochaguliwa kuwa wazee na mashemasi ili kuangalia mahitaji ya kiroho na ya kimwili ya kanisa. Wazee wanapaswa kutazama roho za waumini (Waebrania 13:17): mashemasi kuangalia upande wa mambo ya kimwili (Matendo 6). Tazama kwamba maandiko daima huzungumza juu ya wingi wa wazee na mashemasi katika kila kusanyiko badala ya mzee mmoja na shemasi mmoja kutawala juu yao. Kamwe, wala huwezi kuwa na wazee na mashemasi wa kusanyiko moja kuchukua mamlaka ya kusanyiko jingine, au ya kundi la makusanyiko. Makusanyiko yanapaswa kushirikiana lakini si kutawala jingine.

Maneno; mzee, askofu, mchungaji, na mwangalizi yote hurejea ofisi moja. Hivyo, mzee wa kanisa ni mchungaji, askofu, nk. Katika Tito 1:5-9, Paulo alitaja idadi ya sifa "*Kwa sababu hii nalikuacha Krete, ili uyatengeneze yaliyopunguka, na kuweka wazee katika kila mji kama vile nilivyokuamuru; ikiwa mtu hakushitakiwa neno, naye ni mume wa mke mmoja, ana watoto waaminio, wasioshitakiwa kuwa ni wafisadi wala wasiotii. Maana*

*imempasa askofu awe mtu asiyeshitakiwa neno, kwa kuwa ni wakili wa Mungu; asiwe mtu wa kujipendeza nafsi yake, asiwe mwepesi wa hasira, asiwe mlevi wala mgomvi, asiwe mpenda mapato ya aibu. bali awe mkaribishaji, mpenda wema, mwenye kiasi, mwenye haki, mtakatifu, mwenye kudhibiti nafsi yake; akilishika lile neno la imani vile vile kama alivyofundishwa, apate kuweza kuwaonya watu kwa mafundisho yenye uzima, na kuwashinda wenye kupinga."* Sifa hizi pia zimeelezwa katika, 1 Timotheo 3:1-7. Kwa hiyo si kila mtu katika kanisa anaweza kuwa mzee wa kanisa, isipokuwa ni wale wenye sifa tu ndio waweza kuteuliwa. Hata hivyo, daima lazima kuwepo na uwingi wa watu hawa. Katika makanisa ambapo waumini hawana sifa ya kuwa wazee, watu wa kanisa lazima kushughulikia mambo ya msingi ya kiroho ili kukua na kustawi vya kutosha kwa ajili ya wazee kuteuliwa.

Pia mashemasi wateuliwe kutumika pamoja na wazee. Wao hujulikana kama watumishi na hufanya kazi chini ya uongozi wa wazee wa kanisa. Paulo anaorodhesha Sifa zao, *"Vivyo hivyo mashemasi na wawe wastahivu; si wenye kauli mbili, si watu wa kutumia mvinyo sana, si watu wanaotamani fedha ya aibu. wakiishika siri ya imani katika dhamiri safi. Hawa pia na wajaribiwe kwanza; baadaye waitende kazi ya shemasi, wakiisha kuonekana kuwa hawana hatia. Vivyo hivyo wake zao na wawe wastahivu; si wasingiziaji; watu wa kiasi, waaminifu katika mambo yote. Mashemasi na wawe waume wa mke mmoja, wakiwasimamia watoto wao vizuri, na nyumba zao. Kwa maana watendao vema kazi ya shemasi hujipatia daraja nzuri, na ujasiri mwingi*

*katika imani iliyo katika Kristo Yesu. Nakuandikia hayo nikitaraji kuja kwako hivi karibu”* (1 Timotheo 3:8-13).

Sasa huu ni muundo wa uongozi wa kanisa uliowekwa na Mungu. Kristo ni kichwa, na kila kusanyiko liwe na wazee na mashemasi wake. Chini ya mamlaka yao watakuwepo wahubiri, walimu, na washiriki. Katika njia ya Bwana, kama kusanyiko moja litateleza katika upotofu, wengine wanaweza kuendelea kuwa waaminifu (kama makusanyiko yote watapotoka kasoro moja), basi inawezekana kwao kuwa waaminifu. Katika mpango wa Bwana wa uongozi ni kila ushirika unajiendesha wenyewe au huru kutoka kwa mwingine. Nao hawajafungwa pamoja kwa sheria ya mwanadamu, lakini kwa upendo uliyo katika Kristo. Wanafanya ushirika kati yao, na kufanya kazi pamoja, na kuwa wamoja katika Kristo. Njia zake Kristo haziwezi kuboreshwa.

Hakuna mahali popote katika maandiko unaweza kusoma kuhusu Petro au mtu mwingine yeyote kuwa kichwa cha kanisa. Hakuna mahali utasoma kuhusu askofu au mchungaji kutawala juu ya idadi ya makanisa, au “mchungaji” kuwa kichwa juu ya kusanyiko au kanisa. Wala hakuna mahali utasoma, kuhusu “viongozi wa dini” au “watu wa kawaida”. Sehemu kubwa ya dini za kidunia zimepotoka kutoka muundo wa Mungu wa kanisa, na hiyo ni sababu moja kubwa kwa nini kuna migawanyiko sana ya kidini katika dunia. Hebu na tuamue kurudi katika maandiko ya Biblia kwa vielelezo vya kweli katika maandiko kwa ajili ya muundo wa kanisa.

## MASWALI YA KUJIFUNZA

### Somo la Sita

***Tafadhali toa majibu sahihi kwa maswali yafuatayo:***

1. Nani alianzisha kanisa?

2. Kanisa linaundwa na watu gani?

3. Je, mwili wa Kristo ni wa kimwili au wa kiroho?

4. Je, kuna makanisa mangapi?

5. Kiasili kanisa ni kwa ____________________.

6. Kanisa limeundwa na mamia na maelfu ya ....

7. Je, uongozi wa kusanyiko ni wa mahali pamoja, kitaifa au kimataifa?

8. Je, kanisa la Bwana lina kichwa duniani au makao makuu ya hapa duniani?

9. Nani ni kichwa cha kanisa?

10. Je, viongozi wa kanisa la mahali pamoja wanaitwaje?

11. Ni nini kazi ya wazee wa kanisa na mashemasi?

12. Ni wazee na mashemasi wangapi wapaswa kuwa juu ya kila kusanyiko?

13. Ni majina gani mengine wanaitwa wazee wa kanisa?

14. Ni wapi zimetajwa sifa za wazee wa kanisa?

15. Zimetajwa wapi sifa za mashemasi?

16. Je, kusanyiko linaweza kuwa na wazee wa kanisa na mashemasi hata kama hakuna washiriki wenye sifa za kuteuliwa?

17. Katika hali hiyo, nani analiongoza kanisa?

18. Ni kwa jinsi gani makusanyiko huunganishwa pamoja?

19. Je, muundo wa kanisa wa Mungu unaweza kuboreshwa?

20. Je, Petro ni kichwa cha kanisa, kulingana na maandiko?

21. Je, tunasoma katika maandiko juu ya ofisi katika kanisa ambapo mtu mmoja aitwaye askofu kutawala juu ya idadi ya makusanyiko kadhaa?

22. Je, tunasoma kuhusu mchungaji kuwa juu ya kanisa moja?

23. Je, tunasoma katika Biblia juu ya walio muhimu na wasio muhimu?

24. Kwa nini kuna mgawanyiko sana katika ulimwengu?

25. Wapi tunapaswa kwenda kupata mfano wa muundo wa uongozi wa kanisa?

7

# SOMO LA SABA

# KUINGIA KATIKA KANISA



Katika masomo yetu hadi kufikia sasa tumeweza kuona umuhimu wa kanisa. Hii inaungwa mkono na ukweli kwamba maandiko hufundisha kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya kanisa (Waefeso 5:25), ambalo yeye alilinunua kwa damu yake mwenyewe (Matendo 20:28), na kwamba yeye ni Mwokozi wetu (Waefeso 5:23). Maswali haya yanaibuliwa: Je, Kristo alikufa kwa ajili ya kitu ambacho si muhimu? Je, angemwaga damu yake kununua kanisa lisilo na faida? Je, anaweza kuwa Mkombozi wake na mtu akaokolewa akiwa nje yake? Hakika ungependa kusema hapana kwa kila moja ya maswali haya, na sawa ndivyo. Hivyo kwa nini inasemwa kanisa si muhimu na mtu anaweza kuokolewa bila hata kuwa mshiriki wake? Kwa sababu tu watu hao hawajapata kuelewa kanisa nao wamedanganyika katika fikra.

Hakika Biblia haifundishi kwamba kanisa ni Mkombozi, lakini wakati huo huo huwafundisha kwamba ni lazima mtu kuwa ndani ya kanisa ili kuokolewa. Kama vile safina haikuwa Mwokozi, lakini Nuhu na familia yake iliwapasa kuwa ndani ya safina ili wapate kuokolewa kutokana na gharika, ndivyo ilivyo kwa kanisa. Si hivyo tu lakini mtu akiokolewa Bwana humwongeza katika kanisa. Wakati watu waliposikia injili na kutii siku ya Pentekoste, na siku zilizofuata, maandiko yanasema, "*wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa"* (Matendo 2:47). Hivyo kama mtu ameokoka yeye ni mshiriki wa kanisa la Bwana. Kama yeye si mshiriki, basi hajaokoka. Ni rahisi hivyo. Kwa maneno mengine, hakuna kitu kama kuokolewa nje ya kanisa. Mtu anaweza kuokolewa bila

kuwa mshiriki wa dhehebu au vikundi vya imani za watu, lakini pia hawezi kuokolewa bila kuwa mshiriki wa kanisa la Kristo.

Tukiendelea kujifunza tunaona kuwa mtu hawezi kujiunga na kanisa la Bwana. Badala yake, Bwana anaongeza waliokolewa katika kanisa lake. Kama Bwana huowaongeza waliokolewa tu katika kanisa, basi kanisa limeundwa na wale waliookolewa tu. Bwana hutazama moyo, nia, nk., ambayo inazaa vitendo vya mtu kuona kama yupo na moyo wa dhati kutii. Kama kweli anania sahihi, basi Mungu humwongeza katika kanisa. Kama sivyo, Mungu hawezi kumwongezi hata kama unaweza kumkiri, maana yeye amekwenda kwa njia ya vitendo vya nje tu, na kwa kuwa hatuwezi kuona nia ya ndani ya moyo wa mtu. Kama mtu anaweza kujiunga na kanisa, wote watakubalika bila kujali nia zao. Hii ndiyo sababu Bwana anawajibika kwa kila ongezeko. Yeye hufanya bila makosa kuwa ni nani awe miongoni mwa waliookolewa na ambaye hupita tu katika mfumo.

Kwa kuwa Kristo ni Mwokozi wa kanisa, naye anawaongeza wale waliookolewa tu, mtu anaweza kutaka kufahamu Bwana anahitaji nini mtu afanye ili mtu apate kuongezwa. Hii imewekwa wazi na maneno ya Mungu katika maandiko. Hasa imewekwa wazi katika mazingira ya waongofu kadha wa kadha katika kitabu cha Matendo. Lakini angalia mambo ya msingi au hatua za kuingia katika kanisa la Bwana;

1. Ni lazima mtu kusikia ukweli (Warumi 10:17)
2. Ni lazima tumwamini Mungu na Kristo (Yohana 14:1)

3. Lazima atubu dhambi zake (Luka 13:3)
4. Lazima kumkiri Kristo kuwa Mwana wa Mungu. Kristo mwenyewe asema. *"Basi, kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, nami nitamkiri mbele za Baba yangu aliye mbinguni."* (Mathayo 10:32).
5. Na ni lazima abatizwe kwa ondoleo la dhambi zake. Ubatizo huu ni kuzikwa katika maji (Warumi 6:3,4: Matendo 8:26-39), *"Aaminiye na kubatizwa ataokoka,asiyeamini, atahukumiwa"* (Marko 16:16), *"Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe lika mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, Mpate ondoleo la dhambi zenu, Nanyi mtapkea kipawa cha Roho Mtakatifu"* (Matendo 2:38).

Sasa tumejifunza nini mwanzoni mwa somo hili? Tuligundua kwamba Bwana anaongeza wale waliookolewa tu katika kanisa. Hii inamaana kwamba mtu akimtii Bwana ataokolewa, na moja kwa moja anaongezwa katika kanisa. Tumekwisha ona kwamba kwa kusikia ukweli, kuamini, kutubu dhambi, kumkiri Kristo, na kubatizwa, mtu anaokolewa. Hivyo, mtu akiyafanya hayo huongezwa katika kanisa, kwa vile kumtii Mungu ni mpango ambao kwao tunaweza kuokolewa, na kisha Bwana ataongeza katika kanisa.

Njia nyingine ya kueleza hili, ni kwamba Bwana alisema kwa njia moja tu twaweza kuingia katika ufalme wa Mungu ni kwa njia ya kuzaliwa kwa maji na kwa Roho (Yohana 3:3-5). Lakini ufalme ni nini? Je, ni kanisa (Mathayo 16:18-19). Je, Bwana ana njia mbili kwa mtu kuingia katika kanisa? Hakika sivyo. Kwa hiyo,wakati mtu anaamini na kubatizwa (kwa kuzaliwa na Roho

kwa njia ya neno na kisha kutii mafundisho yake) mtu huyo amezaliwa katika ufalme wa Mungu, au familia ya Mungu, ambayo ni kanisa la Bwana.

Tena, Paulo anasema kwamba, tunabatizwa katika mwili moja (1 Wakorintho 12:13). Lakini mwili huo ni upi? Ni kanisa (Wakolosai 1:18). Kuna miili mingapi? Kuna mmoja tu (Waefeso 4:4, Waefeso 1:22-23). Jinsi gani mtu huingia katika huo mwili? Kupitia kubatizwa. Kristo anasema kwamba ni lazima mtu kuamini na kubatizwa ili apate kuokolewa (Marko 16:16). Hivyo ndivyo Wakorinto walifanya (Matendo 18:8). Kwa hiyo wakati mtu anabatizwa katika kanisa anakuwa sehemu yake au anaongezwa katika kanisa.

Kuna njia moja tu ya kuokolewa, kama tulivyoona, Bwana anaongeza waongofu tu katika kanisa. Je, wewe ni mshiriki wa kanisa lile unalolisoma katika Biblia? Kama siyo, basi wewe haujaokolewa. Chunguza, jifunze, na hatimaye kumtii Bwana wetu Yesu Kristo, naye binafsi atakuongeza katika kanisa lake.

# MASWALI YA KUJIFUNZA

## Somo la Sita

***Tafadhali toa majibu sahihi:***

1. Tumeona nini katika kujifunza kwetu kuhusu kanisa?

2. Nani alikufa kwa ajili ya kanisa?

3. Kanisa lilinunuliwa kwa nini?

4. Ni nani Mkombozi wa kanisa?

5. Jinsi gani tunajua kwamba kanisa ni muhimu?

6. Kwa nini baadhi husema kwamba kanisa si muhimu?

7. Je, kanisa linaokoa?

8. Je, ni lazima mtu kuwa mshiriki wa kanisa ili kuokolewa?

9. Nuhu na familia yake walipaswa kuwa wapi ili kuokolewa kutokana na mafuriko?

10. Kulikuwa na wokovu wowote nje ya safina?

11. Nani aliongeza waliookolewa ndani ya kanisa?

12. Toa mstari wa andiko unaofundisha juu ya hayo.

13. Kama mtu akiokolewa moja kwa moja anakuwa mshiriki wa kanisa gani?

14. Je, mtu aweza kujiunga na kanisa la Bwana?

15. Ni hatua gani tano ambazo mtu apaswa kuchukua ili aweze kuongezwa katika kanisa?

16. Je, mtu anaweza kuokolewa bila kutii amri hizi?

17. Ubatizo ni nini?

18. Ni nini makusudi ya ubatizo?

19. Ufalme ni nini?

20. Ni kwa njia ipi na ya kipekee, inayoweza kumuingiza mtu katika ufalme?

21. Mwilli ni nini?

22. Kuna miili mingapi?

23. Jinsi gani mtu anaweza kuingia katika huo mwili?

24. Kuna njia ngapi za kuokolewa?

25. Kuna njia ngapi za kuingia ndani ya kanisa?

# 8

## SOMO LA NANE

# IBADA YA KANISA



Kanisa limeundwa na waliookolewa. Makusudi yake ni kumwabudu na kumtumikia Mungu kwa njia ya Yesu Kristo. Paulo alisema, "*Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye"* (Wakolosai 3:17).

Kuna aina tatu za ibada zilizoainishwa katika Agano Jipya. Kwanza, tunasoma juu ya ibada ya ujinga. Wakati Paulo akiwa katikati ya kilima cha Mara huko Athene, aliona sanamu nyingi, akasema, "*Kwa sababu nilipokuwa nikipita huko na huko na kuyaona mambo ya ibada yenu, naliona madhabahu iliyoandikwa maneno haya, kwa Mungu asiyejulikana. Basi mimi nawahubirini habari zake yeye ambaye ninyi mnamwabudu bila kumjua"* (Matendo 17:23). Kama walivyokuwepo wale walioabudu kwa ujinga katika kipindi kile, vivyo hivyo wengi hufanya hivyo hata leo. Si tu kuna mamilioni wanaopiga magoti kusujudia sanamu na picha, lakini wapo mamilioni wengi zaidi hufuata shughuli mbalimbali za kidini kwa ujinga au kutoelewa maandiko.

Pili, neno la Bwana lina zungumza juu ya wale wafanyao ibada za bure. Kristo alisema, "*Nao waniabudu bure, Wakifundisha mafundisho Yaliyo maagizo ya wanadamu"* (Mathayo 15:9). Watu wengi huabudu kwa namna hiyo leo. Wao humwabudu Bwana, ni kweli, lakini ibada yao ni bure au utupu kwa sababu hufanywa kwa kufuata mafundisho na tamaduni za watu badala ya imani na mapenzi ya Mungu.

Tatu, neno la Mungu linaongea juu ya ibada ya kweli, iliyo katika Roho na kweli. Tunasoma maneno ya Kristo,

“*Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli”* (Yohana 4:24). Hii ni aina pekee ya ibada ambayo Mungu anaikubali. Hii ilikuwa ni kweli katika siku za Kristo na ni kweli katika siku zetu za sasa. Hii ni ibada inayoelekezwa kwa Mungu katika Roho (kwa unyenyekevu na uelewa) na katika kweli (kama ilivyoandikwa). Mungu hamlazimishi mtu yeyote kumuabudu lakini wale wanaomwabudu lazima kufanya hivyo kama yeye alivyoagiza.

**1. Wao walikusanyika ili kujifunza**. Ingawa Timotheo amekuwa akifundishwa maandiko kutoka utoto (2 Timotheo 3:15), Paulo alimhimiza kama mhubiri kijana, “*Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli”* (2 Timotheo 2:15). Hii inaweza kutumika kwa Wakristo wote na hasa kama wakusanyikapo kwa ajili ya ibada. Katika Matendo 20:7 tunasoma mahubiri ya Paulo kwa ndugu zake kama njia ya kujifunza neno la Mungu.

**2. Waliomba**. Baada ya watu kumtii Bwana siku ya Pentekoste, tunasoma, *“wakawa wakidumu katika fundisho la mitume,na katika ushirika na katika kuumega mkate, na katika kusali”* (Matendo 2:42). Kupitia maombi ya watu wa Mungu wanapata nafasi ya kuzungumza na Baba yao Mbinguni. Ni Mkristo gani hufikiria kukusanyika na Wakristo wengine bila kushiriki katika ibada ya maombi?

**3. Waliimba nyimbo za sifa.** Paulo aliandika kwa ndugu zake, “*mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni*

*mwenu;"* (Waefeso 5:19). Pia soma Wakolosai 3:16 na Waebrania 13:15. Kuna aina mbili za muziki. Moja ni kwa sauti asili na nyingine ni vyombo. Ni aina gani ya muziki Mungu anataka? Anataka muziki wa sauti za asili. Paulo alisema na tumwimbie Bwana mioyoni mwetu. Hii inaondoa muziki wa vyombo. Wakristo wa kwanza waliimba sifa kwa Mungu. Karne chache baadaye waliongeza muziki wa vyombo, lakini Mungu hakutaka hivyo na wala Mungu hatakubali. Wakristo hawawezi kumsifu Mungu kwa muziki wa vyombo zaidi kuliko wanavyoweza kumsifu katika sala na nyimbo za sifa.

**4. Walikusanyika kushiriki meza ya Bwana**. Tuna mfano wa haya katika Matendo 20:7. Katika Mathayo 26:26-28 na 1 Wakorintho 11, tunafundishwa kushiriki mkate katika kukumbuka mwili wa Kristo na kwamba tutashiriki kikombe, au matunda ya mzabibu, katika kumbukumbu ya damu ya Kristo. Na kwamba yatupasa kufanya hivyo hata leo.

**5. Walitoa fedha zao.** Paulo aliamuru ndugu katika Galatia na katika Korintho "*Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake, kwa kadiri ya kufanikiwa kwake; ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja;"* (1 Wakorintho 16:2). Pia soma 2 Wakorintho 9:7. Wakristo wale wa mwanzo walikutana katika siku ya kwanza ya kila wiki (Matendo. 20:7, 1 Wakorintho 16:2) kumwabudu Mungu. Waliaswa; "*wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia"* (Waebrania 10:25). Wakristo leo yafaa kufanya vitendo hivyo vya ibada siku hiyo hiyo, na kuwa sawa katika kukumbuka.

Ibada ya kanisa ni rahisi sana, kwa uhakika wengi watapotoka katika urahisi wake. Wanafikiri, yapaswa kuwa ndefu na inayotolewa kwa utamaduni sana, kwenda kwa vitendo vile vile, marudio ya sala, nk. Lakini si hivyo. Mungu anaweka wazi mapenzi yake kuhusu ibada na hakupewa mtu kubadilisha hata kidogo. Haiwezi kuongezwa au kupunguzwa bila ya kuwa na laana ya Bwana juu ya wale wanaofanya hivyo. Mungu amesema, na watu wake lazima kutii. Hivyo na kwa hivyo tu Mungu ataabudiwa, atasifiwa, na kuheshimiwa.

***SEHEMU YA KUANDIKIA VITINI***

# MASWALI YA KUJIFUNZA

## Somo la Nane

***Tafadhali toa majibu sahihi:***

1. Kanisa limeundwa na nini?

2. Ni nini kusudi la kanisa?

3. Je, ni nini twaweza kufanya katika jina la Bwana?

4. Tunasoma aina ngapi za ibada katika Agano Jipya?

5. Paulo alikuwa wapi wakati aliona sanamu nyingi?

6. Alisema nini kuhusu ibada yao?

7. Je, kuna watu leo huabudu kwa njia hii?

8. Nani alisema wanafanya ibada yao kwa Mungu bure?

9. Kwa nini ibada yao ilikuwa bure?

10. Toa rejea ya andiko.

11. Je, kuna watu leo ambao ibada zao kwa Bwana ni bure?

12. Ibada ya kweli ni ipi?

13. Dondoa Yohana 4:24.

14. Ni nini maana ya kuabudu Mungu katika roho?

15. Ni nini maana ya kuabudu Mungu katika kweli?

16. Ni aina gani ya ibada ambayo Mungu anahitaji toka kwa watu wake?

17. Tunasoma wapi njia za watu wa Mungu kuabudu?

18. Taja vipengele vitano vya ibada.

19. Je, Mungu anazungumzaje na watu leo?

20. Je, wana wa Mungu wanazungumzaje na Mungu?

21. Aina mbili za muziki ni zipi?

22. Aina gani ya muziki ambayo Mungu anataka?

23. Chakula cha Bwana ni nini?

24. Ni siku gani ya wiki Wakristo hupaswa kukusanyika?

25. Je, mpango wa Mungu wa ibada unaweza kuongezwa au kupunguzwa?

# 9

## SOMO LA TISA

# KAZI YA KANISA



Kwa nini kanisa lipo? Makusudi yake ni yapi? Kazi yake ni nini? Ili kujua, tutakwenda katika neno la Mungu.

Awali ya yote, hebu tuchunguze jinsi kanisa lisivyo kama taasisi za biashara, kuendesha na kufanya shule za kidunia au hospitali. Wala si katika kuchapisha na kuuza vitabu kama biashara kwa lengo la kujipatia fedha. Wakati mambo haya yote yanaweza kuwa mazuri, na Wakristo binafsi bila ya shaka wana haki ya kushiriki katika hayo, kwa ufupi hizo siyo kazi za kanisa. Zaidi na zaidi ulimwengu wa kidini umefika mbali kwa kujikita kwa makini juu ya mambo hayo tena shughuli inapatikana na kuchukua hatua nyingine mbali na mpango wa Biblia na kusudi la Mungu kwa watu wake kuhusu kazi yake.

**1. Akihubiri injili.** Kristo alifundisha mitume, mara tu baada ya ufufuo wake na kabla ya kupaa kwake mbinguni, *"Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari"* (Mathayo 28:19-20), *"Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa"* (Marko 16:15-16). Baadaye Paulo alimhimiza kijana Timotheo, "*lihubiri neno, uwe tayari, wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho*" (2 Timotheo 4:2). Aya nyingine zinaweza kutolewa lakini kimsingi hizi zinaweka wazi uhitaji na mapenzi ya Mungu kwa ajili ya injili kufundishwa.

Kanisa lilifanya nini katika siku za mitume? Washiriki walifanya kama Bwana alivyowataka kufanya. Walihubiri neno. Katika kitabu cha Matendo, kimejaa mifano ya jambo hili. Katika matukio ya uongofu, mahubiri yalikuwa kwa upande wa kufundisha mapenzi ya Bwana. Soma Matendo 2, 8, 9, 10. Lakini ni nani alifanya kazi ya kuhubiri na kufundisha? Baada ya mateso makubwa kuja juu ya watu wa Mungu katika Yerusalemu, maandiko yanasema (Matendo 8:4).

Walihubiri nini? Tena, unachotakiwa kufanya ni kusoma matukio ya waliongolewa katika kitabu cha Matendo na utaona mwenyewe. Lakini kwa ufupi, walifundisha uungu wa Kristo, nini mtu afanye ili aokolewe, umuhimu wa kanisa, vitu vya ibada, umuhimu wa maisha ya Ukristo, nk. Paulo alijumuisha kwa kusema, "*Kwa sababu neno la msalaba kwao wanaopotea ni upuzi, bali kwetu sisi tunaookolewa ni nguvu ya Mungu"* (1 Wakorintho 1:18).

Mbali na kuwa Bwana aliagiza kuhubiriwa kwa ujumbe wake, Paulo anasema imani huja kwa kusikia neno la Mungu (Warumi 10:17). Tena Kristo alisema, "*tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru"* (Yohana 8:32). *"Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwinije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikieje yeye pasipo mhubiri?"* (Warumi 10:14). Yote hii ni kusema watu wamepotea (Warumi 3:23, 6:23), na upendo wa Mungu lazima uhubiriwe (Warumi 5:8), kuonyesha kwamba mwanadamu anaye Mkombozi (Yohana 3:16), na kwamba kwa njia ya utii kwa Mungu mtu anaweza kuokolewa toka dhambini (Warumi 1:16-17; Marko 16:15-16). Wale ambao ni wajinga wa mapenzi ya Mungu au ambao hawana utii watapotea (2 Wathesalonike 1:7-9). Hivyo neno la Mungu lazima lihubiriwe.

**2. Kusaidia maskini.** Tuna mifano katika neno la Bwana likituonyesha kanisa linahusika juu na wale ambao walikuwa katika haja ya msaada, na kwamba lilisaidia kama kulikuwepo na njia ya kufanya hivyo, kama tunavyosoma*, "wakauza mali zao, na vitu vyao walivyokuwa navyo,na kuwagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na haja"* (Matendo 2:45). Hii ilitokana na uhiyari na utashi huru. Lakini tena katika Matendo 6 tunasoma juu ya mgogoro uliokuja juu kati ya Wayunani na Waebrania kwa sababu wajane Wakiyunani walikuwa wanasahauliwa katika shughuli za kila siku. Hivyo mitume waliwaita wanafunzi pamoja na waliwataka nao kuchagua watu saba miongoni mwao ili wapate kuteuliwa kushughulikia hii kazi ya kanisa.

Tunasoma kuhusu Paulo kwenda Yerusalemu kutoa msaada kwa watu maskini huko. Anaendelea kusema, "*maana imewapendeza watu wa Makedonia na Akaya kufanya changizo kwa ajili ya watakatifu huko Yerusalemu walio maskini"* (Warumi 15:26). Hivyo Paulo anaandika kwa nduguze kama Wakorintho*, "Kwa habari ya ile changizo kwa ajili ya watakatifu, kama vile nilivyoamuru makanisa ya Galatia, nanyi fanyeni vivyo hivyo. Siku ya kwanza ya juma kila mtu wa kwenu aweke akiba kwake, kwa kadri ya kufanikiwa kwake; ilikwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja"* (1 Wakoritho 16:1-2).

Nani anastahili kusaidiwa? Kwa kawaida, kwanza kabisa, ni wale wenye uhitaji katika kanisa. Ambao ni, masikini, wazee, wajane, matukio ya dharura, yatima wa Wakristo, na kadhalika. Tunasoma*, "kwa hiyo kadri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote mema; na hasa jamaa ya waaminio"* (Wagalatia 6:10). Lakini si kila mtu afaa

kusaidiwa. Katika 1 Timotheo 5 tunaona kwamba mtu anayestahili kusaidiwa mara kwa mara ni mtu ambaye hana uwezo kujisaidia mwenyewe, ambaye hana ndugu wanaoweza kumsaidia, na mtu anayesaidiwa yampasa kuonyesha kuwa ni Mkristo mwaminifu. Hivyo fedha ya Bwana lazima kutumika kwa makini, na si kutoa tu kwa mtu yeyote anayeomba.

Si tu washiriki wa kanisa wanastahili kusaidiwa lakini pia na watu wote wanaostahili msaada na wasaidiwe, ikiwa tu kanisa lina njia ya kuwasaidia. Soma Yakobo 1:27 na Yakobo 2. Hii ni moja ya njia ya injili kuwafikia watu. Lakini ni wapi tutapata fedha kwa ajili ya kazi hii? Zinatoka kwa washiriki, kama wanatoa kwa hiyari (1 Wakorintho 16:1-2; 2 Wakorintho 9:6-7). Hii ni kwamba kama Mkristo atashindwa kutoa, kanisa halitakuwa na uwezo wa kutoa misaada kwa wale wanaohitaji.

**3. Kuimarisha kanisa.** Kuimarisha maana yake ni kujenga, kutia nguvu, kutia moyo, kuwasaidia washiriki wa kanisa kukua kiroho. Ni mambo gani ambayo hujenga? Neno la Mungu, ushirika, kushiriki katika ibada, kusaidia mtu mwingine, matendo mema, upendo, nk (Soma Matendo 9:31; Warumi 14:19; 1 Wakorintho 8:1; 1 Wathesalonike 5:11; 1 Wakorintho 14:26; 2 Wakorintho 12:19; Waefeso 4:12).

Kwa kumalizia, watu wengi hushangaa jinsi kanisa linavyoweza kufanya mambo haya bila ya mashirika makubwa ya kidunia, bila mtu kama kichwa cha kanisa, na bila harambee maalum. Lakini njia ya Bwana ni njia bora, na ikiwa ni njia moja pekee ya kufanya kazi yake. Mungu anaweza kusifiwa, kuheshimiwa, na kutukuzwa

tu kama tutafanya mapenzi yake na hivyo kutimiza lengo letu kwa kuwa hapa. Kristo ni kichwa cha kanisa na cha kila mshiriki, pamoja na hayo kila mshiriki na afanye sehemu yake. Kanisa linaweza kufanya kazi zake tu kama washiriki hujitoa ili kufanya mambo haya kuwezekana.

Mahubiri husaidia wale wanaohitaji na kuwajenga Waumini. Yote haya ni kwa ajili ya kuokoa roho zilizopotea hadi kufikia mwisho, kusudi Mungu apate kutukuzwa katika mambo yote. Kanisa halina kazi nyingine isipokuwa hii. Siasa, biashara na kugeuza kanisa kuwa kitu cha kusherehesha au cha kijamii ni mambo ya kigeni katika neno la Mungu. Kanisa la Bwana ni mwili wa kiroho, liwe katika ulimwengu au lisiwe ulimwenguni, linatafuta kumtii Mungu na kuwatumikia watu, kubaki kuwa takatifu, kwa wokovu wa washiriki wake wote na kwa utukufu wa Muumba wake. Hili ni kanisa la Bwana, kazi yake, na mpango wake.

## MASWALI YA KUJIFUNZA

### Somo la Tisa

***Tafadhali toa majibu sahihi:***

1. Kanisa la Bwana halipo katika biashara gani?

2. Je, dini za ulinmwengu zipo katika hatia ya kujihusisha na aina mbalimbali za biashara kwa faida?

3. Kazi ya kanisa ni ipi?

4. Eleza agizo la Bwana katika Mathayo 28:19, 20 na Marko 16:16.

5. Eleza Wakristo wa kwanza walivyofanya walipotawanyika katika maeneo mbalimbali.

6. Nini baadhi ya vitu walivyovihubiri?

7. Imani huja kwa njia gani?

8. Nini hutufanya kuwa huru?

9. Awezaje mtu kuokolewa?

10. Nani atapotea?

11. Je, kanisa lina husika na wale walio katika haja ya msaada?

12. Nani alichangia kwa mahitaji ya watakatifu maskini katika Yerusalemu?

13. Je, ni kila mtu anayestahili kusaidiwa?

14. Kundi gani la watu linastahili kusaidiwa kwanza?

15. Eleza mipaka kwa ajili ya kusaidia.

16. Je, wale walio nje ya kanisa wafaa kwa kusaidiwa pia?

17. Fedha za kusaidia wale wenye mahitaji hutoka wapi?

18. Lini changizo ikusanywe?

19. Fafanua neno kujenga kulingana na somo hili.

20. Taja baadhi ya mambo yenye kujenga?

21. Jinsi gani Mungu asifiwe na kuheshimiwa?

22. Nani kichwa cha kanisa?

23. Ni nini lengo la kazi ya kanisa?

24. Je, ni kanisa la kidunia?

25. Ni kwa namna gani, siasa, biashara, sio kazi ya kanisa?

*SEHEMU YA KUANDIKIA VITINI*

# 10

## SOMO LA KUMI

# UMOJA WA KANISA



Ulimwengu wa kidini leo unaonekana kujali zaidi juu ya umoja wa kanisa. Harakati nyingi zimeteka usikivu wa watu kila mahali. Sababu kubwa ni kwamba kuna migawanyiko mingi ya kidini katika ulimwengu, na wote wamechoshwa nayo. Lakini bado, umoja kamwe hauwezi kuletwa na makundi ya kidini ya watu yanayo kubaliana kutokubaliana. Migawanyiko bado itakuwepo licha ya ukweli kwamba kuna uwezekano wa kuwapo theluthi flani ya muungano au maelewano. Kwa hiyo, jibu ni nini? Jibu lipo katika Biblia yenyewe. Ili umoja wa kweli uwepo watu lazima kuweka chini mafundisho yao, sheria za imani, majina, makanisa, vitabu vya imani, n,k na kuchukua Biblia, kuisoma na kujifunza, kuiamini, na kutii. Kisha kunaweza kuwa na umoja wa kweli, aina ya umoja ambao Bwana aliombea katika Yohana 17. Watu watakapofanya hivyo, wote wataamini kitu kimoja, kutii mafundisho ya aina moja, wote watavaa jina la kimaandiko, watafanya kazi moja, pamoja watafundisha sawa kila kitu, na wote kwenda Mbinguni pamoja. Itakuwa rahisi sana kwa umoja kuwepo watu watakapoacha kufuata mafundisho ya kibinadamu na kumfuata Kristo.

Maandiko hulaani mgawanyiko. Biblia inasema kwamba, Mungu anachukia wale wanaopanda mgawanyiko au fitina kati ya ndugu (Mithali 6:10). Katika 1 Wakorintho 1 tunaambiwa kuhusu kanisa la Korintho lilivyogawanyika. Badala ya kulaani aina hii ya mambo, mtume Paulo alichukua hatua za haraka kuharibu chanzo cha hayo. Alianza kwa kusema, "*Basi ndugu, nawasihi, kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja*

*na shauri moja"* (1 Wakorintho 1:10). Kisha aliendelea kwa kuuliza maswali matatu, kila moja, lolote kati yake huonyesha matendo yao yasiyo na imani. Maswali yalikuwa: *"Je, Kristo amegawanyika?" "Je, Paulo aliyesulubiwa kwa ajili yenu?" "Au je, mlibatizwa kwa jina la Paulo?"* Katika matukio yote matatu wangeweza kukataa. Kwa hiyo, alionyesha upuuzi wa kugawanyika kwao.

Mtume Paulo huyo huyo aliwaandikia nduguze huko Rumi, "*Ndugu zangu, nawasihi, waangalieni wale wafanyao fitina na mambo ya kukwaza kinyume cha mafundisho mliyojifunza; mkajiepushe nao. Kwa sababu walio hivyo hawamtumikii Bwana wetu Kristo, bali matumbo yao wenyewe; na kwa maneno laini na ya kujipendekeza waidanganya mioyo ya watu wanyofu"* (Warumi 16:17-18). Katika Wakolosai 2:20-23, anasema, "*Basi ikiwa mlikufa pamoja na Kristo mkayaacha yale mafundisho ya awali ya ulimwengu, kwa nini kujitia chini ya amri, kama wenye kuishi duniani, Msishike, msionje, msiguse (mambo hayo yote huharibika wakati wa kutumiwa); hali mkifuata maagizo na mafundisho ya wanadamu? Mambo hayo yanaonekana kana kwamba yana hekima, katika namna ya ibada mliyojitungia wenyewe, na katika kunyenyekea, na katika kuutawala mwili kwa ukali; lakini hayafai kitu kwa kuzizuia tamaa za mwili."*

Yote hii ni kusema kwamba mafundisho ya watu, mafundisho na maagizo ya kibinadamu, huinua watu, kukubaliana na kufuata vitabu vingine tofauti na Biblia, ni mambo ambayo husababisha mgawanyiko. Kwa upande mwingine, umoja unaweza kuwapo na kufurahiwa tu kama watu watamfuata Kristo. Alikuwa ni Kristo ambaye

aliomba, "*Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao. Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma"* (Yohana 17:20- 21). Je, Kristo aliombea yasiyowezekana? Hapana! Basi kwa hakika, umoja unaweza kuwepo. Lini? Wakati sisi tutamfuata Kristo. Mafundisho ya mwanadamu hutugawanya lakini mafundisho ya Biblia hutuunganisha.

Katika Waefeso 4:1-6, tuna kanuni ya umoja. Isikilize, "*Kwa hiyo nawasihi, mimi niliye mfungwa katika Bwana, mwenende kama inavyoustahili wito wenu mlioitiwa, kwa unyenyekevu wote na upole, kwa uvumilivu, mkichukuliana katika upendo; na kujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani. Mwili mmoja, na Roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu. Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja. Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote."* Zingatia kwamba hili ni ombi kwa ajili ya umoja. Tazama pia, kwamba kuna jambo moja kati ya kila mambo yaliyotajwa. Je, kuna mtu amepata hapa kwamba kulikuwa na zaidi ya moja?

Umoja wa kanisa huonekana pale Kristo aliposema atalijenga kanisa lake (Mathayo 16:18), maana ni moja, kwamba ni mwili wake wa kiroho (1 Wakorintho 12:27), na kwamba yeye ni kichwa chake (Wakolosai 1:18). Hakika mtu hawezi kusema Kristo ana miili miwili au

vichwa viwili. Kanisa pia linaonyeshwa kama nyumba ya Mungu au familia ya Mungu (1 Timotheo 3:15). Lakini kuna nyumba au familia ngapi? Moja bila shaka. Tunasoma ufalme wa Kristo au ufalme wa Mungu, pamoja na Kristo kama mfalme (Yohana 3:3-5; Wakolosai 4:11; 1 Timotheo 6:15). Kuna falme ngapi za Bwana na wafalme wangapi? Jibu ni moja tu katika kila upande.

Hakika Biblia inapinga wazo la madhehebu, ambayo yameleta migawanyiko mingi ya kidini. Kwa upande mwingine, huonyesha umoja, ukamilifu, na uzima. Biblia haionyeshi taswira ya kanisa kama chombo kinachoundwa na watu wote wa dini bila kujali imani yao na mazoea. Biblia huonyesha kanisa kama mali ya Kristo. Kanisa linaundwa na wale walioitwa, wale ambao humfuata Kristo na kutii mafundisho yake, na kuokolewa. Kristo hakugawanyika na wala kanisa lake halikugawanyika. Kugawanyika au kuendeleza migawanyiko kwa njia yoyote ni kwenda kinyume na Kristo na yale ambayo aliombea.

## MASWALI YA KUJIFUNZA

### Somo la Kumi

***Tafadhali toa majibu sahihi:***

1. Je, kuna agizo lolote leo juu ya umoja wa kanisa?

2. Nini sababu ya kuwapo haja kubwa ya umoja?

3. Je, umoja unaweza kuletwa na makundi ya kidini yanayokubaliana kotokubaliana?

4. Jibu la kuwa na umoja ni nini?

5. Ni mambo gani wanadamu wanapaswa kuyaacha ili kuwepo na umoja?

6. Nani aliomba ili wote tuwe na umoja?

7. Nini itakuwa matokeo ya umoja?

8. Je, maandiko hulaani migawanyiko?

9. Nani Bwana humchukia?

10. Dondoa 1 Wakorintho 1:10.

11. Taja maswali matatu Paulo aliuliza kwa kanisa la Korintho.

12. Kundi gani la watu wanatakiwa kuwekwa alama?

13. Wanamtumikia nani?

14. Je, tunapaswa kuwaepuka?

15. Ni nani humwabudu Bwana bure?

16. Kristo aliomba nini?

17. Je, aliombea yasiyowezekana?

18. Taja kanuni ya umoja.

19. Yapo mangapi kwa kila moja?

20. Kristo alijenga makanisa mangapi?

21. Kanisa ni nini?

22. Nani ni kichwa chake?

23. Je, Kristo ana mwili zaidi ya mmoja au zaidi ya kichwa kimoja?

24. Bwana ana familia ngapi?

25. Je, neno la Mungu litatugawanya au litatuunganisha?

# 11

## SOMO LA KUMI NA MOJA

# FUNDISHO LA KANISA



Neno fundisho linatokana na neno la Kilatini, [1]credo, na inaelezwa kama, "Aina ya imani, mamlaka, utaratibu wa imani za kidini; au kanuni yoyote au mfumo wa kukiri imani za dini; muhtasari wa kanuni au maoni wanayodai au kuzingatiwa." Mtu anapofikiri kuhusu fundisho kwa kawaida hufikiri kuhusu "Credo (Fundisho) la Mitume" na "[2]Credo (Fundisho) la Nikea." Hata hivyo, hakuna hata moja ya hayo katika Biblia. Aidha, kila kanisa la kibinadamu lina imani yake ya kibinadamu katika mfumo wa vitabu, ufundishaji wa nidhamu, ukiri wa imani, n.k, yote ambayo ni nyongeza katika neno la Mungu.

Labda ipendekezwe kwamba kitabu chochote cha mafundisho ambacho kina maelezo zaidi ya yale yatokanayo na Biblia, kimezidisha. Na kitabu chochote cha mafundisho chenye kupunguza maelezo ya Biblia, basi ni hafifu. Na kitabu chochote cha mafundisho ambacho kina kila kitu kama ilivyo kwenye Biblia basi si kitu kwa sababu tayari tuna Biblia. Ufunuo 22:18-19 na Wagalatia 1:6-9 husisitiza ukweli kwamba hatupaswi kuongeza wala kupunguza neno la Mungu, na sisi si mbadala wake. Kwa maneno mengine, maandiko yamekamilika (2 Timotheo 3:16-17), ni makamilifu (Yakobo 1:25), na sisi hupaswa kusema tu kama maneno ya Mungu (1 Petro 4:11). Kwa hiyo hakuna haja ya kitabu cha ziada au vitabu kama mamlaka.

---

1 "Creed/fundisho" ni andiko la kibinadamu juu ya imani au kuamini kwao.

2 "Credo la Nikea (Nicene) / Imani ya kinikene" ni andiko la imani lililotengenezwa na halmashauri ya kwanza ya Kiekumeni (halmashauri ya Wanikea) karne ya 325 BK ambayo ni tafsiri ya binadamu ya Ukristo."

Ulimwengu wa kidini umegawanyka leo si kwa sababu watu wamefuata neno la Mungu, lakini kwa sababu wao wamekubali mafundisho ya wanadamu. Inasemekana kuwa kila kanisa lazima kuweka mifumo yake, sheria zake, nk. Hii yenyewe ni kukiri kuwa Biblia imeachwa. Jinsi gani inatisha. Hivyo maombi yetu ni kwa kila mtu kuachana na vitabu vya kidunia na kurudi katika Biblia, ambayo ni neno la Mungu. Haitatugawanya bali kutuunganisha katika Kristo Yesu.

Fundisho la kanisa la Bwana ni lipi? Sisi hatuna Mkombozi mwingine isipokuwa Kristo na wala hatuna fundisho isipokuwa Biblia pekee. Maoni yetu na mawazo katika dini hayana maana. Sisi hatuna tafsiri binafsi ya Biblia. Wote tuna Biblia. Tumetii mafundisho yake na kuonyesha wengine. Ombi letu ni kwa watu wote kusoma na kujifunza (Yohana 5:39; 2 Timotheo 2:15), na tunaomba watu kila mahali kufanya yale Biblia inayofundisha.

Sisi hatuna kitabu cha ziada au vitabu ambavyo tunafuata. Hatuamini kwamba kuna watu hai ambao wanaweza kuandika kitabu cha sheria na taratibu ambacho kinaweza kuwa sawa na Biblia. Hatuamini kwamba Bwana amempa mtu mwingine yeyote leo haki ya kuandika kitabu kama Biblia. Hatuamini kwamba Roho Mtakatifu anaongoza mtu mwingine yeyote leo kuandika kitabu hiki.

Ni neno la Mungu na neno la Mungu tu ambalo limetufikia kutoka kwa Mungu, ambalo limevuviwa na Roho wa Mungu, na kwamba linaweza kutuokoa. Aidha, ni neno ambalo Mungu atatuhukumu kwalo siku ya mwisho (Yohana 12:48). Huwezi kupata ukweli isipokuwa kwa

kwenda kwenye chanzo cha kweli. Kwa hiyo kuamini ukweli, lazima kusikia ukweli (Warumi 10:17). Si ajabu kwamba watu wengi wamedanganywa na uongo katika mambo ya kidini. Si ajabu kwamba kuna mgawanyiko sana na machafuko katika ulimwengu wa kidini. Watu wamekwenda kwa mwanadamu kwa ajili ya msaada badala ya Bwana. Mtu akageuka na mafundisho ya watu badala ya maandiko ya Biblia. Hakika, basi mtu lazima kuirudia Biblia kama anataka kuokolewa.

Tunataka kuhamasisha watu kuiendea Biblia ili kujifunza ukweli kuhusu kanisa. Kuna makanisa mengi bandia katika dunia. Lipi ni la kweli? Je, mtu anaweza kufanya utafiti na kuweza kuyatofautisha kila moja? Hapana, mtu na apaswa kukiendea kitabu ambacho kinasema ukweli kuhusu kanisa. Mara baada ya yeye kujifunza ukweli kuhusu kanisa la Bwana, hatakuwa na shida kuliona ambalo hufuata mafundisho ya Biblia.

Tunataka kuhamasisha watu kuiendea Biblia kujifunza ukweli kuhusu kile mtu anapaswa kufanya ili kuokolewa. Kuna njia nyingi za kuokolewa, kwa mujibu wa mafundisho ya wanadamu, lakini wakati mtu ataendea kitabu cha Mungu yeye anaona kwamba inampasa mtu kusikia ukweli, kuamini, kutubu dhambi zake, kumkiri Kristo, na kubatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi zao (Marko 16:15-16; Matendo 2:38). Ni tofauti gani inafanywa na kile wanadamu wanachosema? Bwana ndiye anayeokoa, na hivyo ni lazima mtu kusikia na kumtii ili kuokolewa. Tunapaswa kuhimiza mtu kuiendea Biblia kujifunza jinsi ya kumwabudu Mungu. Kinyume na kile watu wanachosema, kuna njia nyingi za kuabudu.

Biblia inafundisha kwamba kuna njia moja tu na Bwana aliielekeza katika neno lake (Yohana 4:24).

Si tu juu ya mambo haya, lakini juu ya yale yote yanayohusiana na wokovu na uzima na utauwa, tunataka kuwaomba watu wote kuiendea Biblia kwa ajili ya ukweli kuhusu hilo. Ikiwa mtu anabaki na hisia kwamba Biblia haiwezi kueleweka, na dhahiri haiwezi kueleweka sawasawa, hii si kweli. Shetani hupenda mtu kukaa mbali na Biblia ili apate kupotea. Lakini kuokolewa lazima kuiendea Biblia, kuiamini hivyo, na iwe njia yake moja kumwongoza katika masuala ya dini. Kisha ni katika hayo, tu aweza kuokolewa, kwa sababu tu amekuwa na haki.

Mafundisho yetu ni yapi? Yesu Kristo na neno lake. Tofauti na hapo hakuna nyingine. Tunaamini kwamba Kristo ni Mwana wa Mungu na kwamba ujumbe wake ni wa mwisho. Kwa sisi kukubali na kumfuata peke yake. Tunawaomba wengine wote kufanya hivyo. Mafundisho ya mwanadamu yatakuongoza kwenda sehemu moja tu, Jehanamu. Yesu alisema, "*Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi*" (Yohana 14:6).

# MASWALI YA KUJIFUNZA

## Somo la Kumi na Moja

***Tafadhali toa majibu sahihi:***

1. Elezea, fundisho ni nini.

2. Ni kitu gani kila kanisa la kibinadamu (dhehebu) huwa nacho?

3. Eleza ni nini kitatokea kwa wale ambao wanaongeza au kuondoa kutoka neno la Mungu.

4. Je, maandiko yapo kamili?

5. Iliyo kamili ni nini?

6. Je, twapaswa kunena nini?

7. Je, kuna haja yoyote ya vitabu vya ziada ya mamlaka?

8. Kwa nini ulimwengu wa kidini umegawanyika leo?

9. Je, Biblia hutugawanya?

10. Fundisho la kanisa la Bwana ni lipi?

11. Je, mawazo yetu binafsi yana thamani yoyote katika imani?

12. Je, tuna haki ya kufanya tafsiri zetu binafsi?

13. Je, kuna watu leo ambao wangeweza kuandika kitabu ambacho kitakuwa sawa na Biblia?

14. Bwana ametoa haki kwa mtu yeyote, haki ya kuandika kitabu na kudai kuwa ni sawa na Biblia?

15. Neno la Mungu lilitoka wapi?

16. Neno gani litatuhukumu siku ya mwisho?

17. Ukweli ni nini?

18. Wanadamu wamekimbilia ukweli wa nani?

19. Ni kitabu gani twapaswa kukiendea kujifunza ukweli kuhusu kanisa?

20. Je, kuna njia nyingi za kuokolewa?

21. Biblia inafundisha nini mtu anapaswa kufanya ili kuokolewa?

22. Je, Bwana ameweka wazi katika neno lake kwamba ni nini inatupasa kufanya katika ibada?

23. Je, Biblia inaweza kueleweka?

24. Je, wote twaweza kuelewa Biblia sawa?

25. Nani ni njia moja na njia pekee ya mbinguni?

# 12

# SOMO LA KUMI NA MBILI

# HISTORIA YA KANISA



Katika Matendo 2 mazingira yanaonyesha kuanzishwa au mwanzo wa kanisa la Bwana au ufalme. Mitume wapo Yerusalemu, Roho anamwagwa juu yao, mataifa mengi yamewakilishwa kwani walikusanyika kwa ajili ya Pentekoste. Petro na mitume wengine watangaza kwamba hii inatimiza lile lililonenwa na nabii Yoeli, Kristo amefufuka kwa hivyo siku za mwisho zimeanza. Toba na ondoleo la dhambi lahubiriwa, watu 3000 wakaguswa na mahubiri ya injili na kubatizwa, na Bwana akawazidisha katika kanisa lake. Kisha kutoka Yerusalemu injili ikaenda Yudea, juu ya Samaria na hatimaye mwisho wa dunia mpaka kila kiumbe chini ya mbingu wamesikia (Matendo 1:8; Mathayo 28:19-20; Marko 16:15-16; Wakolosai 1:23).

Kanisa liliongezeka na kukua katika siku za mitume na kuenea kwa kasi. Baada ya uongofu wa Paulo, alifanya safari tatu, si tu kuhubiri injili kwa Wayahudi pekee, bali kwa watu wa Mataifa mengine pia. Matokeo yake watu wengi waliweza kuamini na makusanyiko mengi ya kanisa la Bwana yalianzishwa katika Asia na Ulaya. Lakini hii haikuwa rahisi, kwa kuwa kulikuwa na mateso mengi. Kwanza, kanisa lilianza kupata mateso katika Yerusalemu. Kwa sababu hii wanafunzi walitawanyika, walikwenda kila mahali na kuhubiri neno (Matendo 8:1-4). Kadri mudu ulivyoendelea, Warumi waliwalaumu Wakristo kwa matatizo yao mengi na kuweka eneo maalum la mchezo wa kuwaadhibu katika maeneo yote ya Rumi. Hatimaye Paulo alifungwa na kupelekwa Rumi ili kushitakiwa. Historia ya ulimwengu inatuambia kwamba mitume wote isipokuwa Yohana waliuwawa kifo cha kunyongwa kwa sababu ya Kristo. Mamia na maelfu

na pengine labda mamilioni ya Wakristo pia walipoteza maisha yao.

Licha ya mateso, kanisa lilikua na kuenea tu. Haikuwa pigo na mateso kwa kanisa yaliyosababisha ukuaji huu, bali ni mambo yaliyofanyika ndani ya kanisa kama vile kulihubiri kanisa kila mahali lenyewe. Mtume Paulo alitabiri siku ambayo kungekuwa na anguko kubwa. Kwa maneno mengine, alikuwa akisema kuwa itakuja siku ambayo wengi wa washiriki wa kanisa la Bwana wataanguka katika makosa. Lakini hebu na tuchunguze anachokisema, "*Basi, ndugu, tunakusihini, kwa habari ya kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo, na kukusanyika kwetu mbele zake, kwamba msifadhaishwe upesi hata kuiacha nia yenu, wala msisitushwe, kwa roho, wala kwa neno, wala kwa waraka unaodhaniwa kuwa ni wetu, kana kwamba siku ya Bwana imekwisha kuwapo. Mtu awaye yote asiwadanganye kwa njia yo yote; maana haiji, usipokuja kwanza ule ukengeufu; akafunuliwa yule mtu wa kuasi, mwana wa uharibifu; yule mpingamizi, ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa; hata yeye mwenyewe kuketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu. Je! Hamkumbuki ya kuwa wakati nilipokuwapo pamoja nanyi naliwaambieni hayo? Na sasa lizuialo mwalijua, yule apate kufunuliwa wakati wake. Maana ile siri ya kuasi hivi sasa inatenda kazi; lakini yuko azuiaye sasa, hata atakapoondolewa. Hapo ndipo atakapofunuliwa yule asi, ambaye Bwana Yesu atamwua kwa pumzi ya kinywa chake, na kumwangamiza kwa ufunuo wa kuwapo kwake; yule ambaye kuja kwake ni kwa mfano wa kutenda kwake Shetani, kwa uwezo wote,*

*na ishara na ajabu za uongo, na katika madanganyo yote ya udhalimu kwa hao wanaopotea; kwa sababu hawakukubali kuipenda ile kweli, wapate kuokolewa. Kwa hiyo Mungu awaletea nguvu ya upotevu, wauamini uongo; ili wahukumiwe wote ambao hawakuiamini kweli, bali walikuwa wakijifurahisha katika udhalimu"* (2 Wathesalonike 2:1-12).

Wakati akizungumza na wazee wa kanisa huko Waefeso, Paulo alisema: "*Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe. Najua mimi ya kuwa baada ya kuondoka kwangu mbwa-mwitu wakali wataingia kwenu, wasilihurumie kundi; tena katika ninyi wenyewe watainuka watu wakisema mapotovu, wawavute hao wanafunzi wawaandamie wao. Kwa hiyo kesheni, mkikumbuka ya kwamba miaka mitatu, usiku na mchana, sikuacha kumwonya kila mtu kwa machozi"* (Matendo 20:28-31).

Kama Paulo alivyoonya, kulikuwa na wale wa kutoka ndani ya kanisa waliojitokeza na kuanza kupotosha wengi waliokuwa wakimfuata Kristo. Historia ya ulimwengu inatuambia kwamba kuanguka kulianza na mashambulizi ya serikali, au taasisi hii ya ushirika wa kanisa. Mpango wa Bwana ulikuwa kwamba kila ushirika ulipaswa kuwa huru juu ya watu wengine pamoja na wazee wake wenyewe na mashemasi. Hata hivyo, muda ulivyo pita makanisa haya yalianza kuinua mzee mmoja au askofu juu ya wengine, na hatimaye kuruhusu mmoja wa maaskofu hawa kutawala juu ya makanisa kadhaa, matokeo haya yalipelekea baadaye mmoja kuteuliwa kuwa askofu

juu ya kanisa zima. Hii haikutokea mara moja tu, bali kwa kipindi cha miaka mingi, na hivyo karne ya 606 BK (Baada ya Kristo) kwa mara ya kwanza kukawa na Askofu Mkuu, au Papa, sehemu ya ukengeufu wa kanisa, na kusababisha Kanisa Katoliki kama tunavyolijua leo. Ni nini kilichotokea kwa kanisa la Bwana? Waaminifu wachache katika kanisa lake Kristo waliendelea, pengine hata bila kutambuliwa kwa ujumla. Hata hivyo, Bwana aliahidi kwamba ufalme wake au kanisa litasimama milele, na hivyo ndivyo ilivyo kuwa, na ndivyo ilivyo.

Kama ulimwengu wa kidini ulivyo, Kanisa Katoliki lilitawala. Na kwa kweli lilitawala dunia kwa kipindi cha takribani miaka iliyojulikana kama zama za giza. Hii ni kwa sababu Kanisa Katoliki lilikataa kuruhusu Biblia kusomwa na watu wa kawaida, likisema kuwa makuhani tu ndio walionasifa ya kusoma na kuelewa Biblia, na hivyo waliwaambia watu yale yanayofundishwa na wao. Kwa kawaida hii inamaana kwamba waliwaambia watu vitu vile walivyotaka watu wajue. Sio yale yaliyonenwa na Mungu katika Biblia.

Katika kipindi hiki hata Kanisa Katoliki liligawanyika katika Rumi na matawi ya Kiyunani juu ya mafundisho kama ubatizo wa kunyunyiza na muziki wa vyombo. Na muda ulivyozidi kwenda, Kanisa Katoliki kupitia mabaraza yake, nk, liliongeza mafundisho mengine mengi nakuimarisha mifumo yake ya imani. Hatimaye katika miaka ya 1500 Kanisa Katoliki lilikuwa limeshapotoka kiasi kikubwa kwa mafundisho na kimaadili. Hii ilipelekea mtu kwa jina la Martin Luther kutaka kufanya matengenezo ya kanisa, yeye mwenyewe alikuwa kuhani katika Kanisa Katoliki wakati huo.

Hata hivyo, alitengwa, na aliliacha kanisa na kwenda kufundisha na kutenda kile alicho dhani kwamba ni sawa. Kwa kupitia hayo yalikuja yale yaliojulikana kama harakati za matengenezo, au Uprotestanti, na kwa kupitia haya yalikuja madhehebu tuliyonayo leo. Uamuzi wa Luther ulianzisha majaribio mbalimbali katika maeneo mengi ya dunia kutaka watu kurudi katika mafundisho ya Biblia. Licha ya hayo, hawakufanikiwa kikamilifu.

Katika miaka ya elfu moja mia nane na elfu moja mia tisa kulikuwa na watu wa madhehebu katika Ulaya na Marekani waliochoshwa na migawanyiko na machafuko ya kimadhehebu. Taratibu wakaanza kuondokana na makosa waliyokuwa nayo na kuanza kurudi kikamilifu katika Biblia. Makusudi yao hayakuwa kuanzisha kanisa jipya bali walitaka kurudi katika kanisa moja ambalo wanalisoma katika maandiko. Walifanya hivyo, na tangu wakati huo hitaji la Ukristo safi wa Agano Jipya umesomwa katika Biblia na kueleweka duniani kote na mamilioni huondokana na mafundisho ya wanadamu na kuwa Wakristo au washirika wa kanisa la Bwana, wakiwa na Biblia tu kama kiongozi wao pekee.

Wakristo, walikwenda katika maeneo yote ya ulimwengu na kuhubiri ukweli. Wakristo wamegundua kanisa bado lipo katika usafi wake tayari katika maeneo yote kama vile Afrika, India, Russia, Poland, na maeneo mengine mengi. Kanisa hilo lipo leo kama lilivyo wahi kuwepo. Si lazima kuchunguza tangu mwanzo ili kuthibitisha kwamba ni kanisa moja la Biblia. Kielelezo cha kanisa kipo katika Biblia na wakati tukikifuata tupo ndani ya kanisa la Bwana. Mbegu ni neno la Mungu (Luka 8:11) na inazalisha kitu kimoja leo ambacho kilizalishwa

katika siku za Mitume - Wakristo na washirika wa kanisa la Kristo karne ya kwanza. Tunajua ufalme wa Bwana wapaswa kusimama milele. Kwa hiyo umekuwepo mahali fulani tangu siku hizo lilianzishwa na litaendelea kusimama milele, na hakuna mtu wala Shetani mwenye uwezo wa kuliharibu. Huu ni ufalme wa Bwana (kanisa lake) kuwa na ushindi toka mwanzo hadi mwisho na hatimaye kukaa milele zaidi na Bwana Mbinguni.

***SEHEMU YA KUANDIKIA VITINI***

## MASWALI YA KUJIFUNZA

### Somo la Kumi na Tatu

***Tafadhali toa jibu sahihi:***

1. Wapi katika Biblia tunapata hadithi ya kuanzishwa kwa kanisa la Bwana?

2. Lilianzishwa katika mji gani?

3. Watu wangapi waliongezwa katika kanisa kwa wakati huo?

4. Wapi kwingine zilihubiriwa Habari Njema?

5. Safari ngapi za kimissionari Paulo alifanya?

6. Je, Paulo alihubiri kwa Wayahudi tu?

7. Ni katika mabara gani mawili kanisa lilianzishwa kama matokeo ya kazi ya Paulo?

8. Wanafunzi wa injili walifanya nini walipotawanyika ulimwenguni?

9. Nani walilitesa kanisa la Bwana?

10. Mitume wangapi waliuawa kwa sababu ya imani yao?

11. Je, kanisa liendelea kukua licha ya mateso?

12. Je, Paulo alionya nini kingetokea siku za mwisho?

13. Mashambulizi ya kanisa yalianzaje?

14. Kitu gani kilitokea; 606 BK?

15. Ni nini kilichotokea kwa kanisa la Bwana?

16. Kwa nini kipindi cha miaka mia kadhaa kiliitwa zama za giza?

17. Kanisa Katoliki liligawanyika katika matawi mawili, Taja.

18. Taja jina la mtu aliyetaka kufanya matengeneza ya Kanisa Katoliki.

19. Kwa nini alifanya majaribio ya matengenezo?

20. Harakati gani kubwa zilizalishwa na hili?

21. Je, walifanikiwa katika kuirudia Biblia kiukamilifu?

22. Ni nini kilichotokea katika miaka ya 1700 na 1800?

23. Je, watu hawa walianzisha kanisa jipya katika kuirudia Biblia na katika kufuata mfano wa kanisa la Bwana?

24. Je, kanisa hilo moja limepatikana kwa Wakristo katika maeneo mengine ya dunia?

25. Je, kanisa la kweli la Kristo lipo leo?

# 13

## SOMO LA KUMI NA TATU

# KANISA LA LEO



Kanisa la Bwana lilianzishwa takribani miaka elfu mbili iliyopita (Matendo 2) lakini leo lipo vile vile kama lilivyokuwa wakati huo. Unaweza kujiuliza "ni jinsi gani hii inawezekana?" Kwa kifupi ni kwakufuata kielelezo cha Agano Jipya.

Wengine wanahisia kwamba ili kuthibitisha kwamba kanisa la Kristo leo ni sawa kama ilivyokuwa limeanzishwa awali na Bwana tunatakiwa kufuatilia mwaka hadi mwaka katika historia hadi siku ya Pentekoste. Hata hivyo, hii si kweli. Kwanza kabisa, tunaona Bwana akisema kwamba ufalme wake au kanisa lake kamwe halitaharibiwa, na kwamba litasimama milele (Danieli 2:44; Luka 1:33, Waebrania 12:28). Hii inamaana kwamba kanisa lilikuwepo mahali fulani katika ulimwengu tangu mwanzo wake hadi kwenye wakati huu. Na halikupaswa kuwepo kila mahali wakati wote ili kuwa la kweli. Tena, tuna mbegu ya ufalme (Luka 8:11) iliyohifadhiwa katika maneno ya Agano Jipya. Kama ilivyozalisha Wakristo katika siku za mitume, itazalisha Wakristo leo. Kama wale waliokuwa Wakristo katika nyakati za mitume waliunda kanisa, basi hiyo ni kweli hata leo. Hivyo, inawezekana kwa kanisa la Bwana kuwepo popote lilipo Agano Jipya, mradi wale walionalo watafanya kile ambacho kinasemwa nalo.

Mungu daima amewapa watu wake kielelezo cha kufuata. Yeye alimpa Nuhu kielelezo cha kufuata katika kujenga safina (Mwanzo 6). Naye akampa Musa kielelezo cha hekalu, na onyo "*watumikiao mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni, kama Musa alivyoagizwa na Mungu, alipokuwa tayari kuifanya ile hema; maana*

*asema, Angalia ukavifanye vitu vyote kwa mfano ule ulioonyeshwa katika mlima"* (Waebrania 8:5).

Na hivyo katika Agano Jipya tuna kielelezo kamili cha kanisa la Bwana. Kama Nuhu na Musa walivyo tarajiwa kufuata kielelezo walichokuwa wamepewa, vivyo hivyo ni lazima na sisi kufuata kielelezo cha kanisa tulichopewa. Na kama Nuhu na Musa walivyofuata kielelezo cha Mungu kwa ajili ya safina na hekalu, na Mungu alifurahishwa na matokeo, vivyo hivyo nasi tukifuata kielelezo cha kanisa, Mungu atafurahishwa na matokeo kwa vile kanisa litakuwepo tu kama lengo lake. Tufanye bila ya kuongezea wala kupunguza (Ufunuo 22:18-19). Alama zote za utambulisho wa kanisa zimetolewa wazi katika Agano Jipya. Bwana anatuambia kanisa ni nini, nani alianzisha, wapi lilianzishwa, lini lilianzishwa na jina ambalo lilikuwa linajulikana, jina la waumini wake, jinsi ya kuwa mshiriki wa kanisa, ibada yake na kazi yake. Inaeleza nani ni kichwa chake, gharama ya kununuliwa kwake, Mkombozi wake, na kadhalika. Haiachi nafasi ya kuwa na mashaka kama vile ni nini kazi yake. Kielelezo kipo wazi kama neno la Mungu lilivyo wazi.

Basi wote na tunapaswa kujifunza Biblia ili tuweze kujua kanisa moja la kweli la Biblia. Tutakapojifunza ukweli kuhusu hilo na kufuata, basi na tutakuwa washiriki wake (na kuwa kanisa sawa na lile ambalo Kristo alilianzisha). Kama vile ambavyo mbegu huzalisha mazao ya aina yake na neno la Mungu huzalisha Wakristo na washirika wa kanisa la Bwana leo kama ilivyokuwa katika siku za nyuma.

Kanisa la Kristo linaweza kupatikana duniani kote. Lipo hapa na kila mahali. Linaweza kuwepo mahali popote na wakati wowote mtu akifuata kile ambacho Biblia inafundisha na litaacha kuwepo mahali popote duniani ambapo watu wataacha kutenda mapenzi ya Mungu sawa sawa na anavyoagiza katika Biblia au neno lake.

Kanisa la Kristo leo linakua na kuenea kwa kuwa linafuatia Biblia tu. Lina laani mgawanyiko na kumtukuza Kristo bila ya kufuata maandiko. Hili ni kanisa moja unaloweza kulisoma katika Biblia. Siyo dhehebu au mchanganyiko wa madhehebu. Si la Kiprotestanti, si Katoliki, au dhehebu. Bali ni nini? Ni kanisa la Bwana tu. Hivyo tu.

Kanisa la Bwana halina makao makuu ya hapa duniani. Halitukuzi mtu. Halina muundo wa uongozi unaowakilishwa na hekima ya kibinadamu. Kila kusanyiko ni huru pamoja na wazee wake ndani ya muundo wake pamoja na mashemasi, wahubiri, walimu na washiriki. Mjumbe mmoja hana mamlaka wala kutukuzwa juu ya wengine kwa vile kanisa halina watu maalumu au watu wa kawaida.

Kanisa la Kristo daima limekuwa na maadui zake na hivyo lina maadui hata leo. Makundi ya kidini ya watu hulipinga kwa sababu watalikataa kanisa lisilo mfano wake. Wao watalikataa kanisa kwa sababu litakuwa si ushirika wa kweli na kwa kuwaonyesha kuwa hawaendi sawa na mapenzi ya Mungu. Wanatambua kuwa kuna watu hujaribu kufuata Biblia tu, wakati wao wanafuata mafundisho ya wanadamu. Wanatambua kwamba kanisa la Biblia humfuata Kristo tu na tena huvaa jina lake, wakati wao hufuata watu na kuvaa majina ya watu. Silaha

zao dhidi ya kanisa la Kristo si za ukweli, bali mioyo iliyojaa fitina na kupotosha. Lakini kazi yao ni bure.

Kanisa la Bwana limekuwa na ushindi miaka yote. Maadui wote wa dunia hii na pepo wote wa kuzimu hawataweza kulizuia kanisa kukua. Linaweza kuwa na idadi ndogo ya washiriki kwa kulinganisha na wale walizungukao, lakini watakuwa wachache wataokolewa (Mathayo 7:13-14). Kristo ana kanisa moja na yeye atarudi siku moja kwa hilo kanisa moja (Waefeso 5:27; Yohana 14:1-6). Yeye ni mfalme wa ufalme wake na atakuja kwa ajili yake na kumpa Mungu (1 Wakorintho 15:24). Ana bibi arusi mmoja (Ufunuo 21:9) na yeye atakuja siku moja kumpokea huyo bibi arusi mmoja aliyevaa jina lake. Itakuwaje kuhusu watu wengine? Yeye atakiri kwao kwamba kamwe sikuwajua ninyi, atawang'oa (Mathayo 15:13). Watakuwa wamekusanywa na kutupwa motoni.

Ombi letu leo ni kuwa Mkristo safi wa Agano Jipya. Kulirudia neno la Mungu na kulifanya kuwa kiongozi wako. Ijue Biblia, hivyo utakuwa umeijua kweli. Tenda au enenda na neno au Bibla kulingana nayo, nawe utaokoka na kuongezwa katika kanisa la Bwana, moja ambalo unalisoma katika Biblia.

Kama wewe si mshiriki wa kanisa la Kristo tunakuhimiza kuwa mshiriki wake leo. Muamini Mungu, tubu dhambi zako, mkiri Kristo kama Mwana wa Mungu, na kubatizwa ili upate kuokolewa (Marko 16:16; Warumi 10:10; Matendo 2:38). Kisha Bwana atakuongeza katika kanisa lake nawe utakuwa Mkristo (Matendo 2:47; Matendo 11:26). Je, unaweza kufanya hivyo? Hakuna mtu atakuja kukulazimisha kufanya hivyo, lakini kama utajifunza

Biblia yako, tunaamini kwamba wewe utataka tu kuwa Mkristo na hivyo kutumia maisha yako yaliyobaki katika kuishi kwa ajili ya Bwana na kueneza habari zake zinazohusa ufalme wake au kanisa lake.

***SEHEMU YA KUANDIKIA VITINI***

## MASWALI YA KUJIFUNZA

### Somo la Kumi na Tatu

***Tafadhali toa majibu sahihi:***

1. Kanisa lilianzishwa lini?

2. Je, kanisa lipo leo?

3. Lazima mtu aweze kuchunguza historia ya kanisa ya miaka ya nyuma mpaka karne ya kwanza ili kuthibitisha kuwa ndilo kanisa la Bwana?

4. Kwa muda gani Bwana alisema ufalme wake (kanisa lake) utasimama?

5. Mbegu ya ufalme ni nini?

6. Mbegu itazaa nini leo?

7. Elezea Mungu aliwapa nini Nuhu na Musa?

8. Kielelezo cha kanisa la Bwana kipo wapi?

9. Ni zipi alama za utambulisho wa kanisa la Bwana?

10. Bwana anatuambia nini kuhusu kanisa?

11. Jinsi gani tunaweza kujua kanisa moja la kweli la Biblia?

12. Ni wapi tunaweza kuliona kanisa la Bwana leo?

13. Je, kanisa hili ni dhehebu?

14. Je, lina kichwa duniani au makao makuu ya kidunia?

15. Maadui wa kanisa ni nani?

16. Silaha zao ni nini?

17. Kanisa limekua na ushindi kwa miaka yote?

18. Kristo atarudi kuchukua nini?

19. Ombi letu ni nini?

20. Taja hatua ambazo ni lazima mtu kuchukua ili kuwa Mkristo na mshiriki wa kanisa la Kristo.

***Tafadhali zungushia mduara jibu sahihi kama kweli au si kweli:***

KWELI SI KWELI 1. Kanisa ambalo Kristo alianzisha lipo mpaka leo.

KWELI SI KWELI 2. Kuna kanisa moja tu la kweli.

KWELI SI KWELI 3. Limevaa jina la Kristo.

KWELI SI KWELI 4. Mtu apaswa kuwa mshiriki wake ili kuokolewa.

KWELI SI KWELI 5. Kristo atarudi siku moja kwa kanisa lake.

*Nukuu zilizo tumika katika kitabu hiki zimechukuliwa kutoka "Union Version" Biblia ya Kiswahili.*

# MAJIBU

## Somo la Kwanza

**N = NDIYO     H = HAPANA**

1. N
2. H
3. H
4. H
5. H
6. H
7. N
8. N
9. N
10. H

1. Sio dhehebu wala sio dini ya uyahudi, sio ulokole, umoja wa madhehebu, sio taasisi ya kisiasa.
2. Ekklesia
3. Watu waliookolewa
4. Dhana ya ujumla na dhana ya maalum.
5. Yesu Kristo
6. Moja

7. Lililoko Waefeso, Simirna, Pergamo, Thiatira, Sardi, Filadelfia, na Laodikia.
8. Mmoja tu
9. Yesu Kristo
10. Kufanya kazi ya Bwana

1. Neno la kiyunani likimaanisha “walioitwa”
2. Nisawa na kusema.... kanisa la Kristo
3. Familia ya Mungu
4. Kanisa la Mungu
5. Kristo ni mzabibu na Mkristo mmoja mmoja ni tawi, wazo ni kufanya kazi katika shamba la mzabibu na kuzaa matunda kwa ajili ya Bwana.

# MAJIBU

## Somo la Pili

1. Katika mawazo ya Mungu
2. Kabla ya kuweka misingi ya ulimwengu
3. Isaya, Danieli, na Yoeli
4. Milele daima
5. Yesu
6. Kanisa lake mwenyewe
7. Moja tu
8. Nguvu
9. Toba na ondoleo la dhambi
10. Matendo 2

**K = KWELI   S = SI KWELI**

1. K
2. K
3. K
4. K
5. K
6. K
7. K

8. K
9. K
10. K

1. ya kuweka misingi ya ulimwengu
2. siku za mwisho
3. utasimama milele
4. Kanisa langu
5. Yerusalemu

## MAJIBU

### Somo la Tatu

1. Yesu Kristo
2. Mungu kupitia kinywa cha nabii Yoeli
3. Daudi (Matendo 2:34; Zaburi 110:1)
4. Petro
5. Petro

1. Siku za mwisho mwaka 33 baada ya Kristo
2. Yerusalemu
3. Mataifa yote
4. Nguvu
5. Milele

1. Yesu
2. na nguvu
3. toba na ondoleo la dhambi
4. Mataifa Yote
5. Yesu Kristo

1. Mitume
2. uvumi kama uvumi wa upepo ukija kwa nguvu
3. alieleza unabii wa kale uliohusu kuja kwake Yesu

4.a Tutendeje ndugu zetu

4.b Tubuni mkabatizwe mpate ondoleo la dhambi

5. Bwana Yesu Kristo

1. Kanisa - watu walioitwa (kundi la watu)
2. Unabii - kunena mambo yajayo
3. Pentekoste - siku hamsini (50) (Kutoka 23:16; Kutoka 34:22; Hesabu 28:26; Mambo ya Walawi 23:15-19; Hesabu 28:27-29; Kumbukumbu la Torati 16:9-11) (49+1=50)
4. Toba - badiliko la akili, mawazo liletalo badiliko katika matendo (Mathayo 3:8; Matendo 26:18,20; Matendo 3:26; Matendo 17:30; Warumi 2:4; II Kor 7:10; II Petro 3:9)
5. Ubatizo - tosa au zamisha

# MAJIBU

## Somo la Nne

1. Nitakusanya alama zote za utambulisho ndani ya Biblia zinazohusu kanisa
2. Ndiyo yapo
3. Kwa kukusanya alama zote za utambulisho wa kanisa ndani ya Biblia na kulinganisha na alama za kanisa lolote analoliona
4. Ndani ya Biblia
5. Yesu Kristo
6. Yerusalemu
7. Siku ya Pentekoste mwaka 33 baada ya Kristo
8. Kanisa la Kristo
9. ni kanisa
10. Wakristo
11. Yesu Kristo
12. Moja tu
13. Kwanza usikie injili, kuamini, kutubu, kukiri na kubatizwa
14. Kusikia, kuamini, kutubu, kukiri na kisha kubatizwa

15. Sala, kujifunza neno, Chakula cha Bwana, maombi, utoa changizo kwa kadiri ya kufanikiwa kwetu
16. Biblia pekee
17. Wazee wa kanisa
18. Kuhubiri habari njema, kusaidia wahitaji katika kanisa na kuimarisha kanisa
19. Utakatifu
20. Mkristo mwaminifu hata kufa
21. Hapana
22. Hapana
23. Hapana
24. Hapana
25. Katika kanisa lake

## MAJIBU

### Somo la Tano

1. jina
2. makosa, dhambi
3. Yesu, umoja
4. Wakristo
5. Jina jipya

**N = NDIYO H = HAPANA**

1. N
2. N
3. N
4. N
5. H

1. Kuwaenzi wanzilishi wao
2. Uleta mgawanyiko katika imani,uwaenzi wanadamu badala ya Kristo, huwapotosha watu.
3. Umoja
4. Aliwauliza maswali kadha wa kadha mfano ‘Kristo amegawanyika..?

5. Je, mlibatizwa kwa jina la Paulo? Au je, Paulo alisulubiwa kwa ajili yenu..?
6. Kwa sababu Yeye ndo mwanzilishi
7. Salimianeni kwa busu takatifu. Makanisa yote ya Kristo yawasalimu Washirika wa katika kanisa lake
8. Ufalme wa Mungu, nyumba ya Mungu, mwili wa Kristo, n.k
9. Wanadamu
10. Wakristo
11. Matendo 11:26, 1 Petro 4:16, Matendo 26:28
12. Wote watubu
13. Hapana
14. kwa sababu hilo pekee linatuokoa
15. Yote katika kunena na katika kutenda tutende katika jina la Kristo

# MAJIBU

## Somo la Sita

1. Yesu Kristo
2. Waliookolewa
3. Kiroho
4. Moja
5. Kiasili kanisa ni kwa Ujumla
6. Wafuasi au makusanyiko binafsi
7. Mahali pamoja
8. Hapana
9. Yesu Kristo
10. Wazee (maaskofu, waangalizi, wachungaji) na mashemasi kama wasaidizi wa wazee
11. Kulilisha kanisa mahitaji ya kiroho na kulichunga lisiingiliwe na wafundisho ya uongo
12. Ni zaidi ya mmoja
13. Maaskofu,wachungaji, waangalizi
14. 1 Timotheo 3 na Tito 1
15. 1 Timotheo 3:8-13
16. Hapana
17. Wanaume waliopo katika kanisa
18. Kwa neno la Kristo pekee

19. Hapana
20. Hapana
21. Hapana
22. Hapana
23. Hapana
24. Watu wameiacha Biblia pembeni na kuongozwa na mawazo yao
25. Ni katika Biblia pekee

# MAJIBU

## Somo la Saba

1. Kwamba ni lazima mtu awe mshirika wa kanisa hilo ili kuokolewa na kuwa shirika pamoja na Kristo Mwokozi
2. Yesu Kristo
3. Yesu Kristo kwa damu ya Yesu Kristo
4. Yesu Kristo
5. Kristo alikufa kwa ajili ya kanisa lake hilo
6. Hawaelewi tu
7. Hapana, bali kanisa linaokolewa na Yesu Kristo mwenyewe
8. Ndiyo lazima
9. Kwenye safina
10. Hapana
11. Bwana Yesu Kristo mwenyewe
12. Matendo 2:47
13. Kanisa la Kristo
14. Hapana
15. Ajifunze neno la Kristo, amini, atubu, amkiri yesu kuwa Bwana na Mwokozi wake, kisha abatizwe
16. Hapana

17. Ni kuzamishwa au tosa
18. Kuosha dhambi
19. Ni kanisa
20. Kutii fundisho la Kristo
21. Kanisa
22. Mmoja tu
23. Kwa kusikia neno, kuamini, kukiri, kutubu, na kubatizwa
24. Moja tu
25. Hatua 5

# MAJIBU

## Somo la Nane

1. Washirika
2. Kuhubiri injili
3. Kwa kutenda au neno tufanye katika jina hilo
4. Aina 3
5. Athene
6. Wanaabudu wasicho kijua
7. Ndiyo wapo
8. Yesu Kristo
9. Walifuata mafundisho ya wanadamu
10. Mathayo 15:8, 9
11. Ndiyo wapo
12. Ya katika kweli na katika Roho
13. Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli
14. Mawazo na akili viwe kwa Mungu
15. Unachofundisha na kutenda vitokane na neno la Kristo
16. Katika roho na kweli
17. Katika Biblia

18. Kuimba, kuomba, kujifunza neno, meza ya Bwana, na changizo
19. Ndiyo
20. Kwa njia ya maombi
21. Sauti ya asili na sauti ya vyombo
22. Sauti ya asili
23. Mkate na kikombe kwa ajili ya ukumbusho wa Bwana wetu Yesu Kristo
24. Siku ya kwanza ya juma
25. Hapana

# MAJIBU

## Somo la Tisa

1. Ya kujipatia fedha au kipato kwa faida ya kimwili
2. Ndiyo
3. Kuihubiri injili, kusaidia maskini, na kuwahimalisha Wakristo (au kanisa).
4. Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri injili, aminiye na kubatizwa ataokolewa
5. Wakalihubiri neno la Bwana
6. Ufalme wa Bwana, yaani kanisa lake Kristo, toba na ondoleo la dhambi n.k
7. Kusikia neno la Kristo
8. Neno la Kristo
9. Kwa kusikia, kuamini, kutubu, kukiri, na kubatizwa
10. Asiyeamini maneno ya Kristo
11. Ndiyo
12. Kanisa au washirika wa kanisa la Bwana
13. Hapana, isipokuwa wale wahitaji
14. Wale wahitaji katika kanisa
15. Kanisa linapaswa kusaidia wale wenye uhitaji tu, wasio jiweza.

16. Sio kila mtu anaye omba.
17. Kwa washirika wake Kristo, vile wanavyojitoa kwa kadri ya kufanikiwa kwao
18. Siku ya kwanza ya jumaa
19. Kutiana moyo, kumsaidia Mkristo mwenzio akue kiroho
20. Neno la Kristo, ushirikiano, kuhuzulia ibada, kusaidiana, kazi nzuri, upendo, n.k.
21. Tukifanya mapenzi Yake
22. Yesu Kristo
23. Kuokoa roho za watu
24. Hapana, ni la kiroho
25. Kwa sababu kanisa sio la kidunia, utafuta kumpendeza Mungu katika yote. Lipo duniani lakini sio la kidunia.

# MAJIBU

## Somo la Kumi

1. Ndiyo
2. Ili wote tunene mamoja
3. Hapana
4. Wote waache mafundisho na mapokeo ya wanadamu na kuiendea
5. Biblia kiukamilifu
6. Mafundisho na mapokeo ya wanadamu
7. Yesu Kristo
8. Wote tutakuwa na imani moja inayo fundishwa na Mungu katika Biblia
9. Ndiyo
10. Anaye leta mgawanyiko katika imani na tutoheshimu Neno Lake
11. Basi ndugu, nawasihi, kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwa nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja.
12. Kristo amegawanyika? Mlibatizwa kwa jina la Paulo?
13. Paulo alisulubiwa kwa ajili yenu..?
14. Kundi la wale wafanyao fitina
15. Wanamtumikia Shetani

16. Ndiyo
17. Wafundishao uongo
18. Umoja
19. Hapana
20. Kutii kweli ya Kristo
21. Moja
22. Moja tu
23. Watu walioitwa
24. Yesu Kristo
25. Hapana
26. Moja tu
27. Litatuunganisha

# MAJIBU

## Somo la Kumi na Moja

1. Ni aina flani ya imani
2. Imani ya kibinadamu
3. Wataadhibiwa na Bwana kwa kuongezewa mapigo
4. Ndiyo
5. Biblia
6. kweli ya Kristo
7. Hapana
8. Hawataki kuongozwa na kitabu cha Mungu (Biblia)
9. Hapana
10. Maandiko matakatifu ya Mungu (Biblia)
11. Hapana
12. Hapana
13. Hapana
14. Hapana
15. Mbinguni...Kwa Mungu mwenyewe
16. Neno la Kristo
17. Neno lake Kristo
18. Wa wanadamu
19. Biblia

20. Hapana
21. Asikie injili, amini, atubu, akiri, kisha abatizwe
22. Ndiyo
23. Ndiyo
24. Ndiyo
25. Yesu Kristo

# MAJIBU

## Somo la Kumi na Mbili

1. Matendo 2
2. Yerusalemu
3. Watu 3,000
4. Yudea, Samaria na ulimwenguni kote
5. Safari 3
6. Hapana, alihubiri hata kwa mataifa pia
7. Asia na Ulaya
8. Walilihubiri neno (injili)
9. Warumi
10. Wote isipokuwa mtume Yohana
11. Ndiyo
12. Anguko kubwa
13. Ndani ya kanisa
14. Askofu mkuu akachaguliwa
15. Waaminifu wachache walibaki na imani
16. Watu hawakuruhusiwa kusoma Biblia
17. Tawi la Rumi na tawi la kiyunani
18. Martin Luther
19. Alitaka watu wairudie Biblia

20. Watu walichoshwa na migawanyiko
21. Ndiyo
22. Watu wakairudia Biblia na mamlaka yake
23. Hapana
24. Ndiyo
25. Ndiyo lipo

# MAJIBU

## Somo la Kumi na Tatu

1. Takribani miaka 2,000 iliyopita (Matendo 2)
2. Ndiyo
3. Hapana
4. Milele na milele
5. Neno la Mungu
6. Wakristo
7. Aliwapa mfano wa kuufuata
8. Agano Jipya
9. Katika Agano Jipya
10. Anatuambia kuwa kanisa ni nini, nani mwanzilishi wake, mahali lilipoanzia, jina la kanisa, jina la wafuasi wake. Jinsi ya kuwa mshiriki wa hilo kanisa, ibada ya kanisa, kazi ya kanisa, kichwa cha kanisa. Gharama zilizotumika kununuwa kanisa hilo, lini lilianza, na nani Mwokozi wake hilo kanisa.
11. Tusome na kujifunza Biblia pekee.
12. Duniani kote au ulimwenguni kote.
13. Hapana
14. Hapana
15. Wale wote wasiotaka kufuata neno la Mungu kama kiongozi wao katika dini na katika kumpendeza

Mungu, bali wao hufuata mapokeo ya wanadamu na nafsi zao wenyewe.

16. Silaha zao sio za ukweli kwani wao hutumia mapokeo ya wanadamu na kuvaa majina yao.

17. Ndiyo

18. Atakuja kwa ajili ya hilo kanisa lake moja. Atakuja kuuchukua ufalme wake ambalo ni kanisa na kumkabizi Mungu Baba.

19. Ombi letu leo ni kuwa Wakristo safi wa Agano Jipya.

20. Kusikia neno la Kristo, kuamini, kutubu, kumkiri Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa kanisa lake tu, na kubatizwa katika maji mengi.

21. Kweli

22. Kweli

23. Kweli

24. Kweli

25. Kweli

# Maelekezo ya Ziada

Sehemu ya majibu katika kitabu hiki imeongezwa Majibu katika kitabu hiki hayajaandaliwa na mwandishi wa kitabu J.C. Choate, bali yameandaliwa na washiriki wa kanisa la Kristo Tanzania.
Tunakusihi tembelea kanisa la Kristo lililo karibu na wewe.

Hiki kitabu kimetafsiriwa baada ya kupata kibali kutoka kwa mwandishi Betty Choate.

Kama utakuwa na maswali juu ya maswali na majibu katika kitabu hiki, tafadhali, wasiliana na Bright Mwakaboko kupitia barua pepe ifuatayo: mwakaboko87@gmail.com au piga 0758 310 304.